




**Uamuzi** mapingamizi mashtaka ya Mbowe kutolewa Jumatatu

UKURASA 3


WHOZU
Uk.12
Nipashe
BT
BURUDANI TELE
JUMAMOSI SEPTEMBA 4, 2021

HUYU NI SHILOLE?
Mwonekano wazidi kutia shaka

MWILI wa mwanamuziki wa Bongo Fleva, Shilole, umezidi kujadiliwa na watu mbalimbali baada ya kuwa na wasiwasi kutokana na unene uliopitiliza.

Baadhi ya wasanii na mashabiki wa muziki kwa wiki sasa wamekuwa wakijadili umbo la mwanamuziki huyo, huku wengine wakimtaka kujiangalia upya kama anataka kuendelea katika muziki.

Katika kilele cha Wiki ya Wananchi, Shilole alipanda jukwaani akiwa amevaa jezi ya timu ya yanga, lakini mwonekano wake wa unene uliopitiliza uliwaacha watu wengi wakiwa katika mshangao.

Baada ya shoo yake hiyo, ndipo watu walipoanza kujadili na kwa maoni tofauti, kuna wale waliomtahadharisha kwa kueleza, lazima afikirie namna ya kupungua na baadhi walimuunga mkono kwa kusema ana haki ya kuwa anavyotaka.

Saidi Juma, amesema unene wa Shilole si jambo baya, lakini anaweza kupata matatizo kama hatachukua mazoezi ya kutosha kuufanya mwili kuwa imara.

"Unapokuwa mnene mwili unapambana na ongezeko la mafuta, ni lazima kupambana binafsi, ili kuufanya kuwa imara na kuweza kufanya kazi kama kawaida," amesema.

Aidha, ameonya kama anataka kuendelea na muziki ongezeko la mwili wake si jambo zuri kwani kuna wakati atashindwa kufanya kazi kama mashabiki wanavyotaka kutokana na kuelemewa na mwili.

Msanii mwenzake, Recho Kizunguzungu, naye amezungumzia hali hiyo kwa kueleza kwamba kunenepa au kupungua ni jinsi mtu mwenyewe anavyotaka.

"Kwenye suala la unene, kunenepa au kupungua ni mtu mwenyewe anavyotaka, Shilole anaishi na mume wake na mumewe ameridhika, mbona hajamwambia aende 'gym' au aende China akajipunguze, ameridhika na mwanamke wake"

UKURASA 11

Nipashe
Jumamosi Septemba 4, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580693
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Gwajima, Silaa kuti kavu CCM


**Yumo** pia Polepole, wahojiwa na kamati ya maadili ya wabunge, hatima yao mikononi mwa Waziri Mkuu .. *Endelea ukurasa 2*



Humphrey Polepole



Jerry Silaa



Askofu Josephat Gwajima

## Askari Magereza mbaroni madai ya kubaka, kulawiti

UKURASA 2

## Maumivu ya tozo maegesho kwa mtandao yaanza rasmi

UKURASA 3

UKURASA WA 2

### ITALIA YATOA MABILIONI KUSAIDIA SEKTA YA AFYA

SERIKALI ya Italia imetenga kiasi cha Euro 1,250,000 za msaada wenye manufaa kwa Tanzania, kwa ajili ya sekta ya afya. Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na Wizara ya Mambo...



UKURASA WA 4

### DART YAFUNGUKA MWENDOKASI KUPITA NJIA

WAKATI Wakala wa Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Mkoa wa Dar ...

UKURASA WA 4

### MATAPELI WATUMIA OFISI YA RAIS KUJIPATIA FEDHA

OFISI ya Rais -Utumishi wa Umma na Utawala Bora, imetahadharisha dhidi ya matapeli wanaotumia...

UKURASA WA 5

### THRDC YABAINISHA UHABA MAWAKILI WANAWAKE

MTANDAO wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), umesema kumekuwa na ushiriki...

MICHEZO POULSEN ATOA SABABU STARS KUISHIKA DR CONGO UK.23 | MAONI, KATUNI UK.6

## Italia yatoa mabilioni kusaidia sekta ya afya

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Italia imetenga kiasi cha Euro 1,250,000 za msaada wenye manufaa kwa Tanzania, kwa ajili ya sekta ya afya.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ujumbe wa madaktari watatu kutoka nchini humo umefanya ziara na kutakutana na uongozi wa Wizara ya Afya, Maendeleoya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Taarifa hiyo ilisema lengo la ziara hiyo ni kuainisha mahitaji na vipaumbele vitakavyoweza kufadhiliwa kwa fedha hizo katika sekta ya afya kwa hospitali zilizopo nchini.

Ujumbe huo unaongozwa na Dk.Davide Bonechi aliyefuatana na Dk. Giulia Dagliana na Dk. Beatrice Borchi, ambao wote ni madaktari kutoka Kituo cha Taifa la Italia cha Afya Duniani.

"Tanzania imekuwa ikishirikiana na Italia katika miradi mbalimbali ya afya nchini, ushirikiano rasmi katika sekta ya afya ulianza mwaka 1968 kupitia Shirika la Madaktari wa Italia-CUAMM-Doctors with Africa," ilisema taarifa hiyo na kuongeza:

"Kuanzia wakati huo, serikali ya Italia imekuwa ikifadhili miradi mbalimbali ya afya kama vile miradi ya kupambana na utapiamlo, afya ya watoto wachanga, afya ya uzazi na kupunguza maambizi ya virusi vya UKIMWI."

Kwa mujibu wa taaifa hiyo, Serikali ya Italia imefadhili miradi ya usafi wa mazingira jijini Dodoma na katika kuunga mkono jitihada za serikali katika utoaji wa huduma za afya, Italia imekuwa ya kwanza kufungua Kituo cha Tiba ya Mifupa na Kituo cha Utafiti wa Magonjwa ya Kuambukiza katika Hospitali ya St. Gaspar, Dodoma.

Taarifa hiyo ilisema vituo hivyo vinaendelea kutoa mchango mkubwa katika kuboresha afya ya wananchi wa Tanzania hususan wakazi wa Dodoma.



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, akizungumza na Balozi wa Ufaransa hapa nchini aliyemaliza muda wake, Frederic Clavier, aliyefika katika Ofisi Ndogo za Wizara, jijini Dar es Salaam jana kwa ajili ya kuaga. **PICHA: WIZARA YA MAMBO YA NJE**

# Gwajima, Silaa wakalia kuti kavu CCM

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAMEKALIA kuti kavu. Ndivyo inavyoweza kuelezwa baada ya wabunge wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Josephat Gwajima (Kawe), Jerry Silaa (Ukonga) na Humphrey Polepole (Kuteuliwa) kuitwa na kuhojiwa na kamati ya wabunge wa chama hicho.

Wabunge hao waliitwa jana mbele ya kamati hiyo ikiwa ni siku chache baada ya Gwajima na Silaa kusimamishwa mikutano miwili ya Bunge baada ya kubainika kukiuka kanuni za bunge kwa kutoa kauli zenye uchochezi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini hapa, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Hassan Mtenga, ambaye ni Mbunge wa Mtwara Mjini, alisema kamati hiyo imemaliza kuwahoji na kuwasikiliza wabunge hao walioitwa kujibu tuhuma zinazo wakabili.

Alisema wabunge hao wanakabiliwa na kosa la kusema uongo na kushusha hadhi na heshima ya Bunge. Alisema baada ya kamati hiyo ya maadili kumaliza kuwasikiliza, itaandaa ripoti ambayo itaipeleka Kamati ya Uongozi wa Bunge ambayo Mwenyekiti wake ni Waziri Mkuu Kassm Majaliwa.

"Hadi Jumatatu ijayo, hii ripoti itakuwa tayari imefika kwenye kamati ya uongozi wa Bunge ambayo ipo chini Waziri Mkuu na majibu yatatolewa. Sisi kazi yetu tumemaliza leo" alisisita Mtenga

Akitolea ufafanuzi kuhusu kuitwa kwa Mbunge Polepole, alisema ni kwa sababu karibu ameonekana katika mitandao ya kijamii akifanya kosa kama alilofanya Gwajima.

"Hivi karibuni mmeona katika mitandao ya kijamii Polepole 'alitweet' kitu kama kilekile alichokua anakifanya Gwajima, ndiyo maana

tumemwita naye katika kamati hii ya maadili ya wabunge wa CCM, kwa ajili ya kumhoji," alisema Mtenga.

Aidha kazi ya kuwahoji wabunge hao ilianza majira ya saa 2:00 asubuhi. Mtu wa kwanza kuhojiwa alikuwa Polepole, ambaye alitoka katika chumba cha kuhojiwa saa 4:47 asubuhi.

Mbunge wa pili alikuwa Silaa, ambaye aliingia saa 5:32 asubuhi na kutoka saa 6:27 mchana mtu wa mwisho alikuwa Gwajima aliyeanza kuhojiwa saa 6:27 mchana hadi saa 8:14 mchana.

Silaa mbele ya kamati hiyo wakiwa wamevalia sare za CCM, ambayo ni suruali nyeusi na mashati ya kijani. Wabunge wote wa CCM, ambao wali-

Baada ya kumaliza kuhojiwa, Polepole alisema kikao hicho ni cha ndani, hivyo hana cha kuzungumza na waandishi wa habari kwa kuwa kamati itatoa taarifa kwa njia zilizowekwa na Chama.

Naye Gwajima alisema anawashukuru waandishi wa habari kuwapo hapo, lakini hana jambo la kuzungumza na anaiachia nafasi kamati kutoa taarifa ya kilichojili.

Silaa kwa upande wake hakutaka kabisa kuzungumza na waandishi wa habari kwa kuwa baada ya kumaliza kuhojiwa, aliingia kwenye gari lake kisha kuondoka.

# Askari Magereza mbaroni tuhuma za kubaka, kulawiti

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Mkoa wa Ilala, linamshikilia askari Magereza Said Hassan (26), mkazi wa Ukonga jijini Dar es Salaam, huku likiendelea kumsaka mwenzake, kwa tuhuma za kumbaka na kumlawiti msichana mwenye umri wa miaka 29 (jina limehifadhiwa).

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Ilala, Debora Magiligimba, alisema Hassan baada ya kubaini anatafutwa na Jeshi la Polisi aliandika ujumbe na kujaribu kujiua.

Alisema ujumbe huo unasomeka: "Mnisamehe bure kwa uamuzi wangu niliouchukua kwa tukio nililofanya nitaonekana nimekufa kizembe."

Akisimulia tukio hilo, Kamanda Magiligimba alisema Jumatano saa 5:30 usiku katika barabara ya Madafu, Ukonga, mtuhumiwa ambaye ni askari Magereza mwenye namba B 9780 WDR Said Hassan akiwa na mwenzake ambaye hajakamatwa, walimkamata msichana huyo.

"Walimkamata msichana huyo kwa nguvu na kumwingiza kwenye gari dogo kisha kuondoka naye hadi nyumba moja iliyopo karibu na Kambi ya KMKM Ukonga Magereza na kuanza kumbaka na kumlawiti kwa zamu," alisema.

Alisema baada ya kumaliza kitendo hicho watuhumiwa hao waliendelea kumfanyia vitendo vya ukatili wa kijinsia na kumsababishia majeraha makubwa na maumivu makali katika sehemu zake za siri.

"Baada ya mtuhumiwa kugundua kuwa anatafutwa na Jeshi la Polisi kwa tukio hili na mwenzake, Alhamis alijaribu kujiua kwa kujinyonga na kuacha ujumbe huo wa maandishi kwa mkuu wake wa kazi na askari mwenzake," alisema.

Kamanda Magiligimba alisema kabla hajafanikisha azma yake ya kujitoa uhai, alikamatwa na kufikishwa kituo cha polisi.

Alisema wanaendelea na msako wa mtuhumiwa mwenzake aliyekimbia baada ya tukio na kumtaka ajisalimishe haraka iwezekanavyo kituo chochote cha polisi.

Kamanda huyo alitoa wito kwa wananchi kuacha kuwatendea wanawake vitendo hivyo vya kikatili na vya udhalilishaji na kuwataka watoe taarifa.

# Uamuzi mapingamizi mashtaka ya Mbowe kutolewa Jumatatu

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, keshokutwa inatarajia kutoa uamuzi wa hati ya mashtaka ya ugaidi yanayomkabili Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, na wenzake watatu kama ina kasoro au la.

Uamuzi huo unatarajiwa na Jaji Elinaza Luvanda baada ya kusikiliza hoja za pande zote mbili zinazopingana, ambzo ni Jamhuri na utetezi.

Upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Robert Kidando, unaiomba mahakama kutupilia mbali mapingamizi ya utetezi unaodai kwamba hati ya mashtaka ina upungufu kwa kuwa hayana msingi.

Wakijibu hoja za mapingamizi hayo jana, mawakili wa serikali Nasoro Katuga akisaidiana na Wakili Kidando, walidai hati ya mashtaka haina upungufu kwa kuwa shtaka la kula njama na ugaidi ni mawili tofauti kwa kuwa kitendo cha washtakiwa kula njama ya kutenda kosa hakikutimia, hivyo ni kosa linalojitegemea kisheria.

Wakili Katuga alidai endapo wangefanikiwa kula njama na kilipua vituo vya mafuta na mikusanyiko kama walivyopanga awali, shtaka hilo lisingewekwa kwenye hati ya mashtaka.

Katuga alidai mashtaka yote yanatofautiana katika hati ya mashtaka na kwamba katika hati ya mashtaka, kuna maneno yameandikiwa washtakiwa walitenda makosa hayo katika eneo na tarehe tofauti tofauti, hivyo hayo ni miongoni mwa maneno yaliyotofautisha mashtaka hayo.

Wakili Kidando alidai sheria ya ugaidi inatoa mlolongo wote wa makosa ya ugaidi na kuna kanuni zinazowaongoza katika kuandaa hati ya mashtaka na zinawasiadia washtakiwa kujua aina ya kosa ambalo wamelitenda.

Alidai katika sheria za Tanzania hakuna mahali ambapo inaainisha lengo la ugaidi kwa kuwa sheria za hapa nchini zimechukuliwa kutoka katika nchi zingine, hivyo msingi wao uliotumika katika kuleta mapingamizi hauna shiko.

Awali, Wakili wa utetezi, Peter Kibatala, alipinga hati ya mashtaka kusomwa kwa madai kuwa ni batili.

Kibatala alidai kitendo chochote kuhusiana na kosa la ugaidi kinatakiwa kuwekwa wazi ili kuunga mkono shtaka la ugaidi kwa mujibu wa maana ya sheria ya ugaidi, kushindwa kufanya hivyo kunafanya mashtaka kuwa na dosari za kisheria zisizoweza kurekebishika, hivyo yaondolewe.

Wakili Jeremiah Mtobesya alidai mashtaka yamejirudia kwa kuwa mashtaka ya kula njama yako mawili na kuna shtaka lingine la kushiki mkutano ambalo pia linajitegemea.

Alidai kufanya mkutano ndicho chanzo cha kosa la kula njama lakini mashtaka hayo yamewekwa yakiwa yanajitegemea kitu ambacho ni kosa, hivyo yanatakiwa kuondolewa ni kosa moja katika mashtaka tofauti.

Katika kesi hiyo, upande wa Jamhuri unawakilishwa na mawakili waandamizi Kidando, Katuga, Ignas Mwinuka, Esther Martin na Wakili wa Serikali Tilimanyo Magige.

Utetezi unawakilishwa na Kibatala, Mtobesya, John Mallya, Jebra Kambole, Frederick Kihwelo, Sisty Aloyce, Selemani Matauka, Nashon Mkungu, Michael Rugina, Bonifasia Makungu, Alex Maseba, Faraja Mangula, Michael Mwangasa na Gaston Shundu.

Washtakiwa katika kesi hiyo, mbali na Mbowe ni Halfan Bwire na Adam Kasekwa, maarufu Adamo na Mohamed Ling'wenya, ambao wanakabiliwa na mashtaka sita.

Katika shtaka la kwanza, wanadaiwa wote, waliku lanjama kati ya Mei Mosi na Agosti Mosi 2020 katila Hoteli ya Aishi, Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro na maeneo mbalimbali ya jiji la Dar es Salaam, Morogoro na Arusha, kulipua vituo vya mafuta kuhatarisha usalama wa Taifa na kusababisha hofu kwa jamii.

Shtaka la pili, wote wanadaiwa kula njama kufanya vitendo vya kigaidi na kutaka kumsababishia majeraha aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengao Ole Sabaya na shtaka la tatu, Mbowe anadaiwa katika kipindi hicho na mahali hapo aliwawezesha kifedha Halfani, Adamu na Ling'wenya huku akiamini fedha hizo zitasaidia katika kufanya ugaidi

kwa kulipua vituo mbali mbali vya mafuta na mikusanyiko kwa lengo la kuharibu misingi ya kisiasa, katiba, uchumi na sifa ya Jamuhuri ya Mauungano wa Tanzania.

Shtaka la nne wanadaiwa kushiriki vikao vya kufanya vitendo vya kigaidi na shtaka la tano, mshtakiwa Adamu anadaiwa Agosti 5 mwaka 2020 eneo la Rau alikutwa na bastora yenye namba A 5340 aina ya Luger.



Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Alphayo Kidata, akizungumza na wafanyabiashara walipakodi wakubwa jijini Dar es Salaam jana, wakati wa mkutano wa kukusanya maoni na kutatua changamoto zinazowakabili. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Maumivu tozo maegesho kwa mtandao yaanza

**Na Salome Kitomari**

WAKALA wa Barabara za Vijijini na Mijini Tanzania (TARURA), imekuja na adhabu kali ikiwamo kufikishwa mahakamani kwa wanaoshindwa kulipa ada ya maegesho kielektroniki na wanaokosea kuegesha vyombo vyao vya usafiri kwenye maeneo ya mijini.

Kipeperushi kilichoanisha adhabu hizo na utaratibu mpya wa maegesho, unarejelea Sheria ya Barabara Namba 13 ya mwaka 2007 pamoja na kanuni zake kuwa unapoandikiwa gharama za maegesho unatakiwa kulipa ndani ya siku saba. "Kuchelewa kulipa ndani ya siku saba, mmiliki wa chombo cha moto anatakiwa kulipia ushuru wa maegesho ndani ya siku saba endapo atashindwa kulipia ndani ya muda atapaswa kulipia mara mbili ya kiasi anachodaiwa," ilisema sehemu ya kipeperushi hicho.

"Kuchelewa kulipa ndani ya siku 14 endapo atashindwa kulipa tozo pamoja na deni analodaiwa kwa muda usiozidi siku 14 atafikishwa mahakamani na akitiwa hatiani atalipa faini ya Sh. 300,000 au kifungo cha miezi 12 au vyote kwa pamoja.

"Hata hivyo, endapo mhusika atakiri kosa ni la usumbufu kanuni itamruhusu wakala kumtoza Sh. 30,000 baada ya kujaza fomu ya kufifilisha kosa.Mmiliki wa chombo cha moto akiegesha chombo cha usafiri vibaya 'wrong parking' atatakiwa kulipa Sh. 30, 000," kiliongeza.

Kwa mujibu wa utaratibu mpya, aliyeegesha gari anatakiwa kulipa ada hiyo kupitia simu ya mkononi, wakala au benki na kinachofanyika ni kuwekewa karatasi ya bili anayodaiwa mhusika akiegesha gari.

Katika stakabadhi inayowekwa kwenye gari mojawapo lilikuwa na namba ya gari, maelezo ya ankara , kiasi cha fedha, namba ya malipo na hali ya malipo ikiwa na tarehe maelezo na kiasi kinachotakiwa kulipwa.

Katika stakabadhi hiyo inamtaka mwenye bili hiyo kuilipa kwa malipo ya serikali kwa kutumia simu au benki ya NMB au CRDB au wakala wa benki husika.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wamiliki wa magari walisema utaratibu huo haujafafanuliwa vyema na kumekuwa na ubambikizaji wa bili husika kwa wanakusanya ushuru huo.

Neema John alisema utaratibu huo unalenga kuhakikisha mapato ya serikali hayapotei lakini unaumiza wenye magari kwa kuwa wanaoweka stakabadhi hizo hawazingatii muda.

"Nimewahi kuegesha gari majira ya saa 12 jioni, alinisubiri hadi saa sita usiku amenikusanyia vikaratasi vingi kwamba natakiwa kulipa, ni vyema ikafafanuliwa muda wa mwisho wa kutoza tozo hiyo," alisema. Pia alisema ni muhimu serikali ikaangalia kwa wanaokwenda kwenye maeneo ya huduma za kijamii kama kanisani, msikitini na hospitali kwa kuwa wanatakiwa kulipia maegesho.

"Ninapokwenda hospitalini siyo kwa kupenda au nakwenda kupata fedha bali ninakwenda kwenye matatizo lakini kwa sasa tunatozwa fedha, hii siyo sawa wenye magari tunaumia sana," alisema.

Naye Patrick Lyimo, alisema tozo hizo ni maumivu makubwa kwa kuwa unapoegedha gari wanafika na kuweka stakabadhi, lakini kuna uwezakano wa kuanza kutokea kamata kamata kwa ambao watalimbikiza.


AJ RECOVERIES LTD
Your vision our future

AJ RECOVERIES LIMITED|REG:141077236|Shekilango sokoni|Ubungo | P. O. Box 1056 | Dar Es Salaam |Tanzania, (Mobile) +255 686153126 : (Mobile) +255 746 336875

## TANGAZO LA NOTISI/MNADA

Kwa idhini tuliyopewa na **LETSHEGO BANK (T)LIMITED– TAWI LA MANZESE** tunatoa notisi ya siku kumi na nne(14) kwa mdaiwa kulipa deni lake, vinginevyo tutauza kwa njia ya mnada wa hadhara dhamana iliyowekwa na mdaiwa/mdhamini kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini;

| S/NO | JINA LA MDAIWA/MDHAMINI | DHAMANA | MAHALI ILIPO | SIKU NA TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | JOELA INVESTMENT COMPANY LIMITED | GARI , SUZUKI CARRY FWD- REG. T 208 DGV | OFISI YA LETSHEGO BANK TAWI LA MANZESE | IJUMAA 17/09/2021 SAA 05:00 ASUBUHI |
| 2. | MASHABELLAH SOUD WOOD/MWALIMU AYOUB SEIF | GARI SUBARU IMPRENZA- REG T 429 DTN | OFISI YA LETSHEGO BANK TAWI LA MANZESE | JUMATATU 20/09/2021 SAA 05:00 ASUBUHI |

**MASHARTI YA MNADA:**

1. Mnunuzi atalipia asilimia 25% ya bei ambayo imefikiwa siku ya mnada na kiasi kilichobaki anatakiwa kumaliza ndani ya siku kumi na nne(14), endapo atashindwa kumalizia salio lililobaki mnada utarudiwa upya na fedha iliyolipwa haitarudishwa. Ukaguzi wa dhamana ni kwa kuwasiliana na dalali au Tawi la benki ya manzese, siku yoyote muda wa kazi.
2. Gharama za kubadilisha umiliki wa dhamana ni ya Mnunuzi.
3. Dhamana itauzwa jinsi ilivyo.

216441602

# Matapeli watumia Ofisi ya Rais kujipatia fedha

**Na Waandishi Wetu**

OFISI ya Rais -Utumishi wa Umma na Utawala Bora, imetahadharisha dhidi ya matapeli wanaotumia jina la ofisi hiyo kujipatia fedha kutoka kwa watumishi wa umma na wananchi wengine.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Utumishi na Utawala Bora, Mohamed Mchengerwa, alitoa tahadhari hiyo jijini Dar es Salaam jana, akibainisha kuwa matapeli hao wamekuwa wakijitambulisha kuwa wanatoka Ofisi ya Mfuko wa Utumishi wa Umma.

Akizungumzia kuibuka kwa wimbi hilo la utapeli kwa watumishi wa umma Mchengerwa alisema uchunguzi wao umebaini watu wanaofanya vitendo hivyo sio watumishi wa umma bali ni matapeli.

"Hawa watu wamekuwa wakiwapigia simu baadhi ya watumishi wa umma wakiwaomba pesa ili wawasaidie watumishi hao kwenye mambo mengi kama vile upandishaji vyeo, uteuzi, kulipwa malimbikizo ya madai yao, uhamisho, ulipaji mafao na uhakiki wa vyeti. "Hawa matapeli wamekuwa wakiwapigia simu watumishi wa umma na kuwaambia watume pesa ili waweze kutatuliwa changamoto hizo.

"Kibaya zaidi wengine wamekuwa wakilaghai watumishi kwa kutumia jina Mheshimiwa Rais, waziri au maofisa mbalimbali waliopo katika Ofisi ya Rais - Utumishi wa Umma," alionya.

Mchengerwa alisema serikali ipo macho na inaendelea kuwasaka matapeli hao, akionya kuwa hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

Alisema watumishi wa umma na wananchi wengine wanapawa kutambua kwamba serikali ina taratibu zake inapotaka kupeleka taarifa kwa watumishi wa umma, hivyo watumishi wanapaswa kuwa makini. Waziri Mchengerwa aliwataka watu wote wanaojihusha na vitendo hivyo vya udanganyifu, kuachana navyo mara moja kwa kuwa Ofisi ya Rais - Utumishi wa Umma kwa kushirikiana na vyombo vingine vya kiserikali wanawasaka wahalifu hao.

"Niwaombe Watanzania ukipigiwa simu na tapeli akajitambulisha kwa mfumo ambao tumeueleza hapo, toa taarifa kwangu na makatibu wakuu. "Hiyo namba ya huyo tapeli aliyokupigia simu unaweza ukaitolea taarifa Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA) kwa kutuma namba hiyo kwenda namba 15040.

"Mtumishi yeyote yule wa umma anayetaka kuwasilisha malalamiko yake serikalini, atatumia namba 02621660240 na hapo atawasiliana na sisi moja kwa moja," alisema.

■**Imeandaliwa na Edwin Mosha (TUDARCo), Irene Mwakatobe (TUDARCo) na Halfani Chusi**



Mwenyekiti wa Tassisi ya Tanzania Tamil Sangham, Balasubramaniyan Venkadachalam (kulia), akikabidhi msaada wa madawati 60 kwa Mwalimu Mkuu wa shule ya msingi Zanaki, Adolph Regoshora, Upanga jijini Dar es Salaam juzi. Shule nyingine zilizonufaika na madawati hayo ni pamoja na shule za msingi za Maktaba na Lumumba. Wengine ni walimu wakuu Emmanuel Patrick Herman wa Lumumba (wa tatu kushoto), Mwajabu Mshana wa Maktaba (wa pili kushoto) na maofisa, Tamil Sangam Karthik Palinisamy (wa pili kulia) na Anandakumar Srinivasan. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TRA yataka mambo tisa kwa wafanyabiashara wakubwa

**Na Halfani Chusi**

MAMLAKA ya Mapato (TRA) imebainisha mambo tisa yanayotakiwa kufanywa na wafanyabiashara wakubwa nchini ili kuleta tija kwa maendeleo ya taifa.

Mamlaka hiyo iliyataja mambo hayo juzi jijini Dar es Salaam wakati wa kikao cha pamoja cha majadiliano kati ya wafanyabiashara wakubwa na maofisa wa TRA, akiwamo Kamishna Mkuu.

Kikao hicho kilikuwa na malengo ya kufahamiana na wafanyabiashara wakubwa, kujadiliana masuala mbalimbali yanayohusu kodi, kujadiliana vikwazo mbalimbali vinavyowakabili wafanyabiashara na kuvitafutia ufumbuzi.

Kamishina Mkuu wa TRA, Alphayo Kidata, katika kikao hicho, aliwataka wafanyabiashara kulipa kodi kwa hiari na kuzingatia utoaji wa risiti kwa wateja wanaonunua bidhaa zao.

Alisema kwa sasa serikali imependekeza mambo kadhaa kwa wafanyabiashara ambayo kama yakifuatwa, yataongeza Pato la Taifa.

"Mambo hayo ni pamoja na: Kuzingatia utunzaji wa kumbukumbu za biashara; matumizi sahihi ya mashine za kielektroniki (EFD); ulipaji kodi kwa hiari; matumizi ya stempu za ushuru; na marejesho ya ushuru wa forodha kwenye sukari ya viwanda.

"Mengine ni: Matumizi ya hati za madai kwa benki; matumizi ya fursa nafuu ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT); kutengeneza na kuwasilisha taarifa ya bei ya miamala baina ya kampuni yenye uhusiano; na mwongozo wa utendaji kazi katika mkataba wa huduma," alisisitiza.

Kamishna Kidata pia alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuufanya umma kuamini kuwa maendeleo ya nchi yataletwa na wananchi wenyewe kwa kulipa kodi kwa hiari.

Baadhi ya wafanyabiashara wakubwa na wawakilishi wa wafanyabiashara wakubwa waliohudhuria kikao hicho, walipongeza serikali kwa kukubali kukaa na kujadili namna ya kutatua kero zinazowakabili sambamba na kupokea ushauri wao.

Khalfani Iddy, Mhasibu Mkuu Bakhresa Food Product, alipongeza TRA kwa uchapakazi na kushauri kuweka mazingira mazuri zaidi kwa wawekezaji.

Iddy pia alisema mamlaka hiyo inapaswa kuhakikisha inashirikiana na mamlaka zingine za serikali ili kuwe na riba nafuu katika mikopo hususan kwa wafanyabiashara.

Mfanyabiashara Godfrey Ferdinand kutoka Kampuni ya Sigara, aliiomba mamlaka hiyo kupita katika kila kampuni kusikiliza kero zao kwa kuwa kuna vilio vingi kutoka kwa wafanyabiashara ambavyo havijibiwi kwa wakati.

## DART yafunguka mwendokasi kupita njia kawaida

**Na Mary Geofrey**

WAKATI Wakala wa Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Mkoa wa Dar es Salaam (DART), ikiendelea kutoa huduma mpya katika njia za Shekilango-Mwenge, Morocco -Mwenge na Morocco- Kawe, mabasi yameonekana yakitembea bila abiria.

DART ilianza kutoa huduma katika njia hizo Agosti 26, mwaka huu kwa kuanza na basi moja na baadaye kuongeza megine mawili huku nauli ikiwa Sh. 400.

Akizungumza na Nipashe, Msemaji wa DART, William Gatambi, alisema njia hizo mpya zimeanza kwa majaribio wakati lengo likiwa ni kupunguza adha ya usafiri kwa wakazi wa maeneo hayo.

Alitaja sababu ya abiria kusuasua kupanda mabasi hayo kuwa ni kuwapo kwa mwingiliano wa mabasi aina ya daladala katika njia hizo.

"Tunaendelea kufanya jitihada za kuhakikisha wananchi wanatumia usafiri huu kwa kutoa elimu kupitia vyombo mbalimbali vya habari kama redio na mitandao ya kijamii," alisema Gatambi.

Alisema huduma hiyo inaendelea kutolewa katika maeneo mengine ambapo mabasi 142 yameendelea kuhudumia njia za Kimara- Kivukoni mabasi 22 na Ubungo-Kivukoni mabasi saba.

Alitaja maeneo mengine na idadi ya mabasi yanayotoa huduma kwenye mabano kuwa ni Moroko-Kivukoni (manane), Kimara –Gerezani (20), Ubungo-Gerezani (sita), Morocco- Gerezani (sita), Kimara-Morocco (manane) na Mbezi- Kivukoni (14).

Gatambi aliendelea kusema pia mabasi mengine yanaenda Mbezi-Muhimbili (saba), Mbezi- Gerezani (15), Muhimbili- Gerezani (matano), Kimara- Mbezi (manane), Morocco-Mwenge (manane) na Mwenge-Shekilango (manane).

Abiria wa Shekilango walilieleza Nipashe kuwa, wanashindwa kupanda mabasi hayo kwa sababu yanasimama muda mrefu tofauti na daladala.Mwanaisha Rashid alisema kusubiria mabasi hayo hadi yajaye ni kupoteza muda wakati watu wanashughuli nyingi za kufanya.

Jumanne Mrisho alisema, "Kama nikilikuta limejaa nitapanda lakini si halijajaa nipande wakati kuna daladala zinakuja zikiwa na abiria na kuondoka haraka."

Mradi huo ulizinduliwa mwaka 2016 ili kupunguza kero za usafiri wa umma hasa kwa wakazi wa pembezoni mwa mji.

Ulianza kutoa huduma kwa wananchi waishio Kimara na Mbezi kuelekea Kariakoo na Posta na baadaye njia nyingine zilianza kupata huduma hiyo.

HABARI KITAIFA

# Jafo aridhishwa udhibiti wa mifumo ya majitaka



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo (wa tatu kushoto), akipata maelezo kuhusu dampo la Chidaya, jijini Dodoma jana, alipofanya ziara ya kukagua utekelezaji wa maelekezo yake. **PICHA: OMR**

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, amezuru kikazi kukagua utekelezaji wa maelekezo aliyoyatoa miezi sita iliyopita katika Dampo la Chidaya na mabwawa ya majitaka eneo la UDOM na Hospitali ya Benjamin Mkapa.

Katika ziara hiyo, Jafo ameonyesha kuridhishwa na utekelezaji wa maelekezo hayo aliyotoa na kutoa rai kwa watendaji wengine wa mamlaka za maji kuhakikisha wanasimamia vyema mifumo ya majitaka ili kulinda wananchi pamoja na mazingira.

Katika ziara hiyo jana, Jafo aliipongeza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (DUWASA) na Halmashauri ya Jiji la Dodoma kwa kusimamia vyema mabwawa ya majitaka na dampo la taka ngumu na majitaka.

Alisema kuwa awali katika ziara yake ya kushtukiza Aprili mwaka huu, alikuta hali isiyoridhisha katika miundombinu hiyo na hivyo kutoa maelekezo kwa Mkurugenzi wa Mamlaka hiyo na Mkurugenzi wa Jiji kuifanyia maboresho ili kulinda mazingira.

"Nimetembelea madampo mbalimbali ndani ya Tanzania likiwamo la Moshi, Arusha mpaka kule Kigoma na maeneo mengine lakini nilikuta hapa changamoto ya usimamizi usioridhisha, hali ambayo endapo mvua ingenyesha yangetiririka kwenye makazi ya watu na kuleta athari za kiafya.

"Sasa leo (jana) nimekuja hapa kufuatilia utekelezaji wa maelekezo hayo nimekuta mmetekeleza mmejenga ukuta ambao utasaidia kuzuia majitaka haya yasitiririke na kuleta athari kwa watu na sio watu tu hata kwa viumbe," alisema Jafo akiwa katika Dampo la Chidaya.

Waziri Jafo aliwataka wasimamizi wa dampo kuhakikisha ukuta waliojenga unadumu kwa muda mrefu ili wananchi wa Dodoma waendeele kuwa salama bila kuathiriwa na majitaka ambayo yangeweza kutiririka wakati wa mvua.

Pia aliwataka wasimamizi hao kulitumia vizuri dampo hilo na kuhakikisha taka zote zinazotupwa huko zinashindiliwa vizuri ili zisisambae ovyo na kuleta uchafuzi wa mazingira.

Mkurugenzi wa DUWASA, Aron Joseph, alimshukuru waziri huyo kwa kutembelea mradi huo mara kwa mara na kutoa maelekezo yake ambayo wameyatekeleza na hivyo hali ya mabwawa kuridhisha.

Akitoa taarifa kuhusu utekelezaji wa maelezo ya awali, Meneja wa Dampo la Chidaya, John Kiwanga, alisema kuwa mara baada ya kupokea maelekezo ya Waziri Jafo kupitia kwa Mkurugenzi wa Jiji, waliyafanyia kazi mara moja na kujenga ukuta huo.

"Kama unavyoona Mheshimwa Waziri, hapa tumejenga ukuta huu kwa matofali ya kawaida tu na hatua hii itasaidia sana kuzuia majitaka kutoka katika dampo hili kutotoka nje na kuchafua vyanzo vya maji," alisema Kiwanga.

# THRDC yabainisha uhaba mawakili wanawake

**Na Beatrice Shayo**

MTANDAO wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), umesema kumekuwa na ushiriki hafifu wa mawakili wanawake katika kesi zenye maslahi kwa umma.

THRDC pia imesema kuna mawakili wanawake 3,055, lakini wanaoshiriki katika kesi za kimkakati ni 92 sawa na asilimia 10 na kwamba kuna pengo kubwa la ushiriki wao.

Akizungumza wakati wa mafunzo ya siku mbili kwa mawakili wanawake, Wakili kutoka THRDC, Leopard Mosha, alisema kumekuwa na ushiriki mdogo wa mawakili hasa wanawake katika kesi zenye maslahi kwa umma na ndiyo sababu ya kutoa mafunzo kwa kundi hilo ili kuwajengea uwezo wa kushiriki kwa wingi kwenye kesi hizo ambazo nyingi ni za kutetea haki za binadamu.

"Taratibu za kisheria ni kwamba kesi zinapofunguliwa mahakamani, mawakili wana wajibu wa kusimamia na kuisaidia mahakama kufikia uamuzi. Kwa hiyo mawakili wanaosimamia kesi hizi zenye maslahi kwa umma wamekuwa wachache hasa wanawake ni wachache zaidi,"alisema.

"Hii ina maana tumekuwa na tatizo kubwa la uwapo wa wanasheria na mawakili wachache wanaotetea haki za binadamu na kusimamia kesi hizi za kimkakati kwa umma. THRDC kwa kushirikiana na wadau wengine wameona kuna haja sasa ya kutoa mafunzo haya ili waweze kufanya kazi zao vizuri," aliongeza.

Pia alisema THRDC inatoa mafunzo hayo ambayo yanakuwa ni endelevu kwa mawakili hao wanawake, ili waweze kufanya kazi zao kwa weledi bila hofu.

Awali, Mwenyekiti wa Chama cha Majaji Wanawake Tanzania, Jaji Joacquine De-Mello, aliwataka mawakili hao kutumia mafunzo hayo kujiimarisha katika kufungua kesi za kimkakati.

"Wito wangu mkitoka hapa ni kutengeneza kundi kubwa la utetezi wa mawakili wanawake, mkifanya maazimio mkubaliane kwamba hili ndio kundi mahsusi lenye nguvu moja ili waondokane na dhana ya kuwa wanawake hawawezi," alisema Jaji De-Mello.

Jaji De-Mello ameipongeza THRDC kwa kuandaa mafunzo hayo, akisema yatasaidia kuongeza ushiriki wa wanawake katika kesi hizo.

Naye Makamu wa Rais wa Chama cha Wanasheria wa Tanganyika, Gloria Kalabamu, amewataka mawakili hao wasikatishwe tamaa na changamoto wanazokabiliana nazo wakati wa utekelezaji majukumu yao.

"Vikwazo vinavyotokea visitukwamishe bali tuyafanyie kazi, mfano unaweza katazwa usifungue kesi ya ndoa za utotoni sababu sio mwathirika lakini unaweza ukatafuta waathirika ukafungua kesi. Hivyo tusirudi nyuma tuwatafute wahusika ili tuwaeleze changamoto tunazopitia," amesema Kalabamu.

halopesa
*150*88#

Ada za wateja
Customer tariffs

| Kiwango (TSH) Range (TSH) | | Ada kwa mteja (Mjumuisho na tozo za Serekali) Customer fee (Inclussive of Government levies) | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kutoka From | Mpaka To | Tuma HaloPesa Send to HaloPesa | Mitandao washirika Other Networks | Tuma kwa namba isiyosajiliwa Send as voucher | Kutoa Pesa Withdraw |
| 100 | 999 | 10 | 10 | - | N/A |
| 1,000 | 1,999 | 30 | 42 | 360 | 310 |
| 2,000 | 2,999 | 31 | 43 | 391 | 311 |
| 3,000 | 3,999 | 69 | 82 | 494 | 419 |
| 4,000 | 4,999 | 94 | 116 | 569 | 539 |
| 5,000 | 6,999 | 200 | 232 | 780 | 850 |
| 7,000 | 9,999 | 218 | 250 | 878 | 868 |
| 10,000 | 14,999 | 544 | 674 | 1,474 | 1,424 |
| 15,000 | 19,999 | 747 | 877 | 1,677 | 1,627 |
| 20,000 | 29,999 | 1,032 | 1,167 | 2,222 | 2,172 |
| 30,000 | 39,999 | 1,140 | 1,328 | 2,390 | 2,370 |
| 40,000 | 49,999 | 1,430 | 1,698 | 2,850 | 3,150 |
| 50,000 | 99,999 | 2,015 | 2,335 | 3,785 | 3,935 |
| 100,000 | 199,999 | 2,471 | 3,121 | 4,521 | 5,071 |
| 200,000 | 299,999 | 2,808 | 3,678 | 6,258 | 6,558 |
| 300,000 | 399,999 | 3,400 | 4,250 | 8,050 | 7,950 |
| 400,000 | 499,999 | 4,070 | 4,850 | 9,470 | 8,870 |
| 500,000 | 599,999 | 4,940 | 6,160 | 11,140 | 10,040 |
| 600,000 | 699,999 | 5,880 | 7,360 | 12,080 | 11,480 |
| 700,000 | 799,999 | 6,370 | 7,850 | 12,620 | 11,970 |
| 800,000 | 899,999 | 7,014 | 8,414 | 13,364 | 12,764 |
| 900,000 | 1,000,000 | 7,980 | 9,380 | 14,530 | 13,730 |
| 1,000,001 | 3,000,000 | 9,580 | 10,180 | 14,880 | 14,080 |
| Zaidi ya 3,000,000 | | 10,000 | 11,500 | 15,300 | 14,500 |

Lipa kwa
halopesa



216441902

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Waamuzi wapigwe msasa wasiharibu ligi msimu mpya

**KLABU** za Ligi Kuu na Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara kwa sasa zipo katika maandalizi makali kuelekea msimu mpya wa 2021/22 utakaofunguliwa rasmi Septemba 25, mwaka huu, kwa mechi ya Ngao ya Jamii kati ya Simba na Yanga itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Baada ya mchezo huo wa Ngao ya Jamii, msimu mpya utaanza rasmi Septemba 29, mwaka huu, ambapo timu 16 msimu huu zitawania ubingwa wa ligi hiyo unaoshikiliwa na Simba kwa misimu minne mfululizo sasa.

Tofauti na miaka iliyopita Ligi Kuu msimu huu inatarajiwa kuwa na ushindani mkali kutokana na historia mpya ya udhamini, iliyowekwa na Kampuni ya Azam Media Limited kwa kuingia mkataba mpya wa haki za matangazo ya Televisheni katika ligi hiyo na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF).

Katika mkataba huo ulioingiwa Mei 25, mwaka huu, utadumu kwa kipindi cha miaka 10 kuanzia msimu ujao wa 2021/22 ukiwa na thamani ya Sh. bilioni 225. 6, ambapo mbali na kiasi hicho, kutakuwa na bonasi kubwa kuanzia bingwa hadi timu itakayoburuza mkia.

Kwa mujibu wa mkataba huo, zawadi za fedha kwa mshindi wa kwanza msimu ujao wa ligi itakuwa Sh.milioni 500, mshindi wa pili milioni 250, watatu milioni 225, wanne milioni 200 na fedha hizo zitakwenda zikipungua hadi timu itakayoburuza mkia huku zile zitakazocheza mechi ya mchujo (play off), kila moja ikilamba Sh. milioni 20.

Hicho ni kiasi pekee kitakachotolewa kutokana na udhamini huo haki za matangazo ya televisheni, ukiacha udhamini wa matangazo ya radio lakini na wadhamini wenza wengine wa ligi hiyo, ikiwamo Benki ya KBC.

Ongezeko hilo la zawadi, limezifanya klabu nyingi kuwa na uhakika wa kuwalipa wachezaji wake, hivyo kuzifanya hata zile zilizokuwa hazifanyi usajili wa wachezaji wakigeni kuingia sokoni kwenye dirisha la usajili lililofungwa rasmi Jumanne saa sita usiku na kusajili nyota kutoka nje ya nchi.

Hilo linatufanya kuamini kwamba ligi ya msimu huu itakuwa na ushindani mkubwa mwanzo mwisho, hivyo ni wakati sasa kwa TFF na Bodi ya Ligi (TPLB) kuwa makini katika usimamizi hususan kwa suala zima la upangaji ratiba ili kutoziumiza baadhi ya klabu.


Mbali na hilo, Chama cha Waamuzi Tanzania (FRAT), hakina budi kuwaandaa waamuzi wake ipasavyo kwa kuzidi kuwapa semina ya kukumbushana kanuni na sheria 17 za soka ili kuchezesha kwa haki na kuondoa malalamiko ambayo tumekuwa tukiyasikia kila msimu.

Tunatambua yapo mabadiliko kadhaa ya kanuni ama sheria za soka ambayo yamefanyika, hivyo ni jukumu pia la kila mwaamuzi kujiongeza kwa kujifunza mabadiliko hayo badala ya kuisubiri FRAT kuandaa semina/darasa kwao, jambo ambalo litawasaidia kutekeleza majukumu yao kwa haki na weledi.

Katika hilo si waamuzi pekee, bali pia kuna haja ya uongozi wa kila klabu kuandaa semina kwa wachezaji wao na kuwaelekeza baadhi ya kanuni zilizobadili ili kuepuka kufanya makosa yasiyo ya lazima, lakini pia kupunguza malalamishi kwa waamuzi pindi ligi hiyo itakapoanza.

Tunatambua wapo wachezaji wengi hata baadhi ya makocha bado hawaelewi baadhi ya kanuni zilizobadilika, jambo ambalo kila uongozi wa klabu hauna budi kutafuta wakufunzi wa soka wabobezi ili kutoa darasa kwa mabenchi yao ya ufundi pamoja na wachezaji, haya yakifanyika kwa makini kuanzia kwa waamuzi, makocha hadi wachezaji, tunaamini tutashuhudia ligi ya viwango zaidi msimu huu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Barnabas Maro

# Maneno ni daraja, hayazuii maji...

**NAAM,** "Maneno ni daraja, hayazuii maji kuteremka." Maana yake daraja haliwezi kuyazuia maji ya mto yasiteremke. Maneno nayo hayawezi kumzuia mtu kufanya jambo aliloazimia (kitendo cha kutia nia ya kufanya jambo; kusudia, dhamiria.)

Methali hii yaweza kutumiwa kumnasihi mtu aliyeazimia kufanya jambo fulani asikate tamaa au asivunjwe na maneno ya watu yasiyoweza kumdhuru kwa namna yoyote. Huweza pia kutumiwa na mtu aliyeazimia kufanya jambo fulani kujitetea dhidi ya maneno ya binadamu.

Unaposoma makala (maandishi kuhusu mada maalumu) hii, zimebaki wiki chache kabla ya kindumbwendumbwe cha Ligi Kuu msimu mpya kuanza. Hata hivyo, wanachama na mashabiki wa timu mbili kongwe nchini wameanza majisifu (maelezo anayotoa mtu ili kujikweza kwa watu; majigambo) kila upande ukisema utatwaa kombe.

Wakati wale wa Simba wakisema watatwaa kombe kwa mara ya tano mfululizo, wenzao wa Yanga wanajibu kwamba kwa kuwa wamechoshwa na mbwembwe (mikogo) ya Simba, msimu huu watawapokonya kombe hilo.

Pamoja na tambo yaani jambo lililofumbika, jambo ambalo utatuzi wake haujulikani; fumbo, mashabiki wa timu hizo mbili kongwe nchini haweshi kutamba mitaani kila upande wakisema watatwaa kombe.

Sisi yetu macho na masikio kwani "mwenye kisu kikali ndiye alaye nyama." Maana yake anayekishika kisu kikali ndiye anayeweza kuikata nyama vizuri. Methali hii yatukumbusha kuwa aliyejiandaa vizuri ndiye anayeweza kufanikiwa katika jambo fulani. Twashauriwa tujiandae ipasavyo kabla ya kuiingilia jambo.

Hata hivyo, wahenga walisema: "Mwenda kasi mngoje achoke." Kwamba haifai kushindana na mtu anayeenda kasi, heri ukasubiri akachoka kwanza, methali hii huweza kutumiwa na mtu mwenye tabia ya kufanya mambo yake kwa papara au pupa na ambaye huishia kuyaharibu.

Kwa hiyo mashabiki wa Simba na Yanga ambao ndio wenye maneno mengi yanayokera wanapaswa kusoma kwa makini methali isemayo: "Mwenye busara mara hunasihika." Maana yake mtu mwenye hekima huufuata ushauri apewao. Hutumiwa kutukumbusha umuhimu na faida za kuyafuata mashauri tuliyopewa na wazazi wetu au na watu wanaotuzidi maarifa.

Yote katika yote, kuanzia msimu huu wa Ligi Kuu nchini, TFF yapaswa kupanga michezo hiyo kwa weledi kuliko ilivyokuwa msimu uliopita kwa timu moja kuwa na viporo vitano, hivyo kurahisisha timu moja kuwa na nafasi ya kufanya vyovyote ili kupanga matokeo ya ushindi!

Vivyo hivyo, waamuzi wanaoshindwa kusimamia haki na weledi wa kufuata kanuni za mchezo bila kufanya upendeleo wa aina yoyote kama ilivyokuwa msimu uliopita. Kwa ajili hiyo TFF iwe makini zaidi kwa waamuzi na wasimamizi wanaokuwa kwenye benchi. Watakaoonekana kushindwa kusimamia vizuri na kwa haki wasimamishwe kama itakavyokuwa kwa waamuzi.

Vilevile TFF yapaswa kuwa na chombo kitwacho VAR yaani 'Video Assistant Referee'. Hiki ni chombo kitumikacho na marefarii itokeapo wachezaji wa upande mmoja kulalamikia bao lililokubaliwa na mwamuzi kuwa halikustahili kwani lilikuwa la kuotea, lilifungwa kwa mkono au mfungaji alifanya kosa kabla ya kufunga.

Ndo maana wahenga walisema: "Kweli ikidhihiri, uwongo hujitenga." Kwamba ukweli unapojulikana uongo unajitenga. Twakumbushwa kwamba ukweli wa jambo fulani utokeapo, uongo unaolihusu hautambuliwi tena au hamna nafasi tena. Huweza kutumiwa kumnasihi mtu anayejaribu kusema uongo wa waziwazi.

Twapaswa kukubali kwamba: "Sheria ni msumeno, hukata mbele na nyuma yaani pande zote." Methali hii huweza kutumika kumpigia mfano mtu anayelalamika kuwa ameonewa kisheria au labda aliyedhania kuwa jambo fulani haliwezi kumfika yeye bali huwafika wengine.

Waamuzi nawaambia: "Halahala mti na macho." Wajifunze au waangalie wasijitie vijiti machoni. Hutumiwa kumpigia mfano mtu anayefanya mambo yake bila uangalifu.

marobarnabas@yahoo.com

**HABARI BUNGENI**

# Mkakati wawekwa ujenzi viwanda vya dawa

SERIKALI imeweka mikakati na mbinu za makusudi kuwezesha uwekezaji wa viwanda vya dawa ili kufikia asilimia 60 ya uzalishaji dawa na vifaa tiba nchini ifikapo mwaka 2025, Bunge liliambiwa jana mjini hapa.

Mikakati na mbinu hizo inahusisha pia kuongeza idadi ya viwanda vya vifaa tiba nchini.

Wizara ya Viwanda na Biashara ilibainisha hayo jana bungeni ilipokuwa ikitoa majibu katika swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Lucy Sabu.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji lini ujenzi wa kiwanda cha vifaa tiba vinavyotokana na zao la pamba mkoani Simiyu utaanza kwa kuwa upembuzi yakinifu ulishafanyika.

Kwa mujibu wa wizara hiyo sekta ya viwanda vya dawa hapa nchini ina jumla ya viwanda 17 ambapo 12 vinatengeneza dawa za binadamu, viwanda viwili vifaa kinga, viwanda viwili dawa za mifugo na kiwanda kimoja cha vifaa tiba.

Ilisema viwanda hivyo 17 vina uwezo wa kuzalisha dawa chini ya asilimia 12 ya dawa zote zinazohitajika nchini na hivyo asilimia 88 ya dawa za binadamu zinazotumika zinaagizwa nje ya nchi.

Aidha, ilisema serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi kwenye sekta hiyo ili kuvutia wawekezaji wengine katika sekta hiyo.

Pamoja na jitihada hizo, ilisema kuna umuhimu pia wa kuanzisha kiwanda cha vifaa tiba Simiyu ambapo malighafi ya pamba inayolimwa kwa wingi nchini itatumika.

Pia ilisema taratibu zote za kuanzisha kiwanda husika zimekamilika ikiwa ni pamoja na upembuzi yakinifu na ujenzi unategemea kuanza mara tu baada ya serikali kukamilisha utaratibu bora wa kugharamia mradi.

# Mbunge ataka 100% mikopo elimu ya juu

MBUNGE wa Chumbuni (CCM), Ussi Salum Pondeza, ameitaka serikali kutoa mkopo wa elimu ya juu kwa asilimia 100 kwa wanufaika bila kujali shule walizosoma.

Akiuliza swali bungeni jana, mbunge huyo pia alihoji serikali inawasaidiaje wazazi waliostaafu ambao wameshindwa kuchangia gharama za elimu ya juu.

Katika majibu yaliyotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, mikopo inayotolewa na Serikali kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu inaongozwa na Sheria ya Bodi ya Mikopo SURA 178 ambayo inaelekeza kuwa walengwa wa mikopo hiyo ni wahitaji.

Aidha, ilisema kwa sasa, uhitaji wa mwanafunzi hupimwa kwa kuchambua taarifa zilizowasilishwa wakati wa maombi ya mkopo, zikiwamo gharama za masomo ya sekondari au stashahada.

Hata hivyo, ilisema uchambuzi huo hutumia king'amua uwezo (Means Testing Tool) ambacho hubaini kiwango cha uhitaji cha mwombaji mmoja mmoja ukilinganisha na wengine.

Ilifafanua kuwa uhitaji wa mnufaika unatumika kuamua kiasi anachopangiwa kulingana na gharama ya shahada aliyodahiliwa na baada ya uchambuzi linganishi, waombaji hupangiwa mikopo kulingana na uhitaji wao.

Katika mwongozo, vigezo na sifa za kunufaika na mikopo ya elimu ya juu, hakuna kigezo mahususi cha shule aliyosoma mwombaji na mnufaika.

Kuhusu waombaji wa mikopo ambao wazazi wao wamestaafu katika utumishi, ilisema serikali inaamini utaratibu wa sasa wa kutambua na kuwapangia mikopo wahitaji wanaotoka katika familia zisizo na uwezo wa kumudu gharama za elimu ya juu kwa watoto wao unajitosheleza.

Ilisema ipo tayari kuendelea kupokea maoni ya namna ya kuboresha zaidi utaratibu huo.



Mbunge wa Jimbo la Fuoni, Abbas Ali Mwinyi, akichangia hoja bungeni, jijini Dodoma juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Gawio serikalini la kampuni hisa chache lafikia bil. 155/-

SERIKALI imeongeza makusanyo yake ya gawio kutoka kampuni ambazo ina hisa chache kutoka Sh. Bilioni 34.92 mwaka 2015/16 hadi kufikia Sh. Bilioni 155.10 mwaka 2020/21. Wizara ya Fedha na Mipango ilibainisha hayo jana bungeni ilipokuwa ikitoa majibu katika swali la Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Jesca Kishoa.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji serikali inatumia mikakati gani kudhibiti mapato yatokanayo na gawio kutoka kwenye kampuni ambayo serikali inamiliki hisa chini ya asilimia 50.

Katika majibu ya wizara hiyo, ilisema kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina ambaye ndiye msimamizi wa uwekezaji wa serikali katika taasisi na mashirika ya umma pamoja na Kampuni ambazo Serikali ina hisa chache.

Pia ilisema inadhibiti mapato yatokanayo na gawio kwa kuhakikisha kuwa kila kampuni ina sera ya gawio, kurejea kwa mikataba ya mauzo ya hisa katika kuhakikisha maslahi ya serikali yanalindwa pamoja na kufanya chambuzi za mara kwa mara kuhusu utendaji wa taasisi hizo.

Aidha, ilifafanua serikali ina uwakilishi kwenye bodi za wakurugenzi wa kampuni ambapo pamoja na mambo mengine husimamia maslahi ya serikali kwenye kampuni ikiwa ni pamoja na malipo ya gawio.

# Simu kutumika kuripoti matukio wanyama wakali

WIZARA ya Maliasili na Utalii imenunua na kusambaza simu zenye namba maalum katika kanda 14 nchini kwa ajili wananchi kutoa taarifa za matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu kwa haraka.

Iliyasema hayo jana bungeni ilipokuwa ikitoa majibu ya swali Mbunge wa Mvomero (CCM), Jonas Zeeland. Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji lini serikali itaondoa wanyama wakali hasa tembo katika Tarafa ya Mlali na kuwarudisha kwenye Hifadhi ya Taifa Mikumi kwa kuwa wamekuwa kero kwa wananchi.

Katika majibu ya Wizara hiyo, ilisema inaendelea kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu hususan Tembo katika Wilaya ya Mvomero, Mkoa wa Morogoro.

Ilisema katika jitihada za kukabiliana na matukio hayo, Wizara kwa kushirikiana na uongozi wa mkoa imeweka mkakati wa pamoja ambapo kuwa na vikosi maalum vya kudhibiti Tembo. Vikosi hivyo vimeendelea kutoa msa

ada wa haraka pale linapotokea tatizo katika Mkoa wa Morogoro ikiwamo wilaya ya Mvomero.

Pia ilisema vikosi hivyo vimepatiwa vitendea kazi muhimu vinavyohitajika katika kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu ikiwamo magari, risasi baridi, risasi za moto na mabomu maalum ya kufukuzia wanyamapori hususani tembo.




**Habari zote na Augusta Njoji,** DODOMA

# Diwani ageuka mbogo wanafunzi kurudishwa

**Na Julieth Mkireri,** CHALINZE

DIWANi wa Mbwewe Halmashauri ya Chalinze mkoani Pwani, Omary Msonde, amewataka walimu wa Shule ya Sekondari Changarikwa, kutowarejesha nyumbani wanafunzi wanaodaiwa fedha ya chakula, badala yake wazazi wawajibishwe.

Msonde alitoa agizo hilo juzi baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa wazazi ambao watoto wao walirejeshwa nyumbani baada ya kushindwa kukamilisha fedha zinazotakiwa.

Alisema zaidi ya wanafunzi 300 walirudishwa nyumbani kwa kushindwa kukamilisha fedha ya chakula na fedha kwa ajili ya mwalimu wa somo la sayansi na rimu moja.

Msonde alisema watoto hao wamekaa nyumbani kwa wiki mbili na baada ya wazazi kutafakari kukosa masomo kwa muda mrefu waliamua kufikisha taarifa kwa diwani huyo ili wapate msaada.

"Watoto walikaa muda mrefu nyumbani na sikuwa na taarifa. Wazazi walinifikishia taarifa baada ya wiki mbili nilipofuatilia waliofukuzwa ni wengi hata wale wanaodaiwa 10,000 jambo ambalo ni kuwakosesha haki ya kuendelea na masomo wakati wanaotakiwa kuwajibika ni wazazi," alisema.

Alisema kwa mwaka mmoja wanafunzi hao wanatakiwa kulipa Sh. 280,,000, kumchangia mwalimu wa sayansi Sh. 15,000 kutokana na shule hiyo kukosa mwalimu wa somo hilo huku kila mmoja akitakiwa pia awe amepeleka rimu moja ya karatasi.

Pia aliwaonya wazazi na walezi wanaoshindwa kutekeleza wajibu wao kubadilika na kuacha kuwa chanzo cha wanafunzi kukosa vipindi vya masomo na kwamba anatarajia kukutana nao kuzungumzia suala hilo na wataoshindwa kuhudhuria watawajibishwa.

Alisema alipopata taarifa za kufukuzwa kwa wanafunzi hao, alikutana na uongozi wa shule na kuzungumza nao kuhusiana na suala hilo, hatimaye walikubaliana wanafunzi kurejeshwa shuleni.

Mmoja wa wazazi aliyejitambulisha kwa jina la Asha Sizya, alimshukuru diwani huyo huku akielezea masikitiko yake kutokana na mtoto wake kukaa nyumba kwa wiki mbili kwa sababu ya kukosa pesa ya chakula.

# Mbunge atoa madawati 1,000 shule za msingi

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MBUNGE wa Morogoro Mjini, AbdulAziz Abood, ametoa madawati 1,000 yenye thamani ya Sh. milioni 52 kwenye shule za msingi 15 zilizoko kata mbalimbali za Manispaa ya Morogoro ili kutatua kero ya uhaba wa samani hizo.

Akizungumza wakati wa kukabidhi madawati hayo kwa nyakati tofauti kwenye shule hizo, Abood alisema hatua hiyo ni utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika kuboresha Sekta ya Elimu ili kuwawezesha wanafunzi kusoma pasi na kuwapo vikwazo.

"Nimetoa madawati haya 1,000 kwa shule hizo ikiwa ni kutatua changamoto ya muda mrefu ya wanafunzi kurundikana katika madawati na wengine kulazimika kukaa chini, hivyo kama mbunge nimeona nisaidie hilo," alisema Abood. Mbunge huyo alisema uamuzi wa kutoa madawati hayo umetokana na kufanya ziara katika shule zote za msingi za Manispaa ya Morogoro na kubaini kero kubwa ya upungufu wa madawati na hivyo kusababisha baadhi ya wanafunzi kukaa chini.

Alisema pamoja na kutoa madawati hayo 1,000 kwa shule hizo 15, ataendelea kutoa madawati mengine kwa shule zingine zilizobaki ili kutatua kero ya uhaba wa samani hizo shuleni.

Katika ziara ya kugawa madawati hayo, Abood pia alibaini kuwapo tatizo la uchakavu wa majengo katika baadhi ya shule zikiwamo za watoto wenye uhitaji maalum na ukosefu wa maji, matundu ya vyoo na umeme.

Aliahidi kukarabati majengo ya shule mbili za watoto wenye uhitaji maalum ikiwamo Shule Kongwe ya Kikundi na Jitegemee huku akitoa mifuko 100 ya saruji katika Shule ya Msingi Juhudi, Kata ya Lukobe kwa ajili uwekwaji wa sakafu.

Mbunge huyo pia alitoa hundi ya Sh. 500,000 kwa Shule ya Msingi Nanenane, Kata ya Tungi kwa ajili ya kulipia deni la maji ambalo walikuwa wakidaiwa huku akitoa mabati 12 na mbao ili kusaidia upauaji wa vyumba vya madarasa mawili na kuingiza umeme kwenye Shule ya Msingi Kiegea iliyoko Kata ya Kihonda.

Baada ya kupokea misaada hiyo, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Nanenane, Deogratius Kimath, alimshukuru mbunge huyo kupatiwa madawati na kulipia bili za maji. Mkuu wa Shule ya Msingi Kikundi, Ndevaulwa Maod, pia alimshukuru Abood kwa kukubali kukarabati majengo na miundombinu ya kitengo cha wanafunzi wenye ulemavu wa akili pamoja na msaada wa madawati.

Diwani wa Mkundi, Sief Chomoka, alipongeza mbunge huyo kwa kusaidia maendeleo ya wananchi katika sekta mbalimbali ikiwamo ya elimu.



Wahitimu wa darasa la saba wa shule ya St. Mary's Tabata, wakiongozwa na walimu wao kuingia kwenye mahafali yaliyofanyika shuleni hapo mapema wiki hii. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Shule yaahidi makubwa kitaaluma

**Na Mwandishi Wetu**

SHULE ya St. Mary's Tabata jijini Dar es Salaam, imeahidi kufanya vizuri kitaaluma kwenye matokeo ya darasa la saba katika mitihani inayotarajiwa kufanyika wiki ijayo.

Hayo yalisemwa hivi karibuni na Mkuu wa shule ya St. Mary's Tabata, Thomas Samson, wakati wa mahafali ya 21 ya shule hiyo yaliyofanyika kwenye viwanja vya shule hiyo.

Alisema walimu wamefanyakazi kubwa ya kuwaandaa wanafunzi vizuri hivyo hawana shaka kuhusu ufaulu mzuri watakaoupata kwenye matokeo hayo.

"Ndugu wazazi naomba niwahakikishie kuwa tumewaandaa vijana hawa kwa uhakika na wote watafaulu vizuri na kwa kuwa tumeshaanza kusajili wanafunzi wa shule ya awali ni vyema mkawaleta wengine," alisema

Mwalimu Samson alisema shule hiyo imekuwa ikifanya vizuri kiwilaya na kimkoa katika matokeo ya kitaifa hivyo aliwasihi wazazi waendelee kuwaamini kwa kuwapeleka watoto wao shuleni hapo.

"Kwenye mtihani wa darasa la saba mwaka jana wanafunzi wetu wote walipata ufaulu mkubwa wa wastani wa daraja A jambo ambalo linatufanya tuwe na imani kwamba mwaka huu pia tutafanya vizuri," alisema

Akizungumza kwenye mahafali hayo, Mkurugenzi wa Shule za St Mary's, Humphrey Rwakatare, aliwashukuru wazazi kwa kuendelea kuiamini shule hiyo na kuwapeleka watoto wao.

Alisema shule hiyo haitawaangusha kwani imeweka mipango kabambe kuboresha huduma za shule hiyo kuanzia usafiri, chakula na miundombinu mingine ili izidi kupaa kitaaluma.

"Tumekuwa tukifanya vizuri kitaaluma mwaka hadi mwaka na tunawaahidi kuendelea kufanya vizuri kitaaluma kwenye mitihani yote ya kitaifa tunaomba tuendelee kushirikiana na mtuletee watoto wenu," alisema.





# Waliochanja corona waitwa kupata vyeti

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imewataka watu waliopata chanjo nchini kijitokeza katika vituo walivyovitumia kuchanja, ili kuchukua vyeti vyao ambavyo vinatolewa kielektroniki.

Mkurugenzi wa Huduma za Kinga wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Leonard Subi, alitoa wito huo jana jijini hapa wakati akitoa taarifa ya upatikanaji wa vyeti vya chanjo ya corona nchini.

Dk. Subi alisema hivi sasa serikali inatoa vyeti vya kielektroniki kwa watu wote, ambao wamekwishapata chanjo katika vituo mbalimbali nchini.

"Watu ambao bado hawajapata vyeti vyao na walishachanja wanatakiwa kwenda katika vituo walivyopata chanjo, ili kupatiwa vyeti vyao ambavyo hivi sasa vinatolewa na serikali kwa mfumo wa TEHAMA.

"Hakuna sababu ya mtu kughushi cheti cha corona kipindi cha nyuma. Tulikamata watu wameghushi vyeti hivi sasa hatutakiwi kughushi kwani tukikukamata tutakupeleka mahakamani kwa kosa la kughushi nyaraka ya serikali na adhabu zake mnazifahamu," alisisitiza Dk. Subi

Pia alisema wizara hiyo imeendelea kuboresha suala la upatikanaji wa vyeti kwa njia ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA), kwa wananchi wenye uhitaji wa vyeti vya kielektroniki.

"Wizara imetoa mafunzo na kuekeleza watoa huduma wanaochanja kuwahudumia wananchi wote wenye uhitaji wa haraka wa vyeti vya kielektroniki katika vituo vyao walipopatiwa chanjo, ambapo watoa huduma wamewezesha kuhakiki na kuingiza taarifa za waliochanjwa kwenye mfumo na kutoa vyeti," alisema Dk.Subi

Kadhalika alisema, ili kuwaondolea usumbufu wananchi waliochanjwa kabla ya mfumo ambao wanahitaji vyeti vya kielektroniki wanashauriwa waende kwenye vituo walipopata chanjo ya corona wakiwa na cheti cha nakala ngumu na fomu waliyojaza ya uhiari.

"Watawapatia watoa huduma, ili kuhakiki na kuwapatia cheti cha kielektroniki, ambapo baada ya kuingizwa kwa taarifa za waliochanjwa watapokea ujumbe mfupi wa maandishi kwenye simu zao za mkononi ambapo ujumbe huo una link inayowezesha kuona na kuchapisha cheti mahali popote," alisema.

# Waziri asisitiza ulinzi kwa watoto wa kike

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

NAIBU Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira na Vijana, Patrobas Katambi, ameitaka jamii kuwalinda watoto wa kike dhidi ya mimba za utotoni, ili wafikie ndoto zao za elimu na maisha.

Katambi alisema hayo jana alipokuwa akizungumza kwenye kikao cha uwasilishaji ripoti ya utekelezaji wa mradi wa kupambana na mimba za utotoni ujulikanao kwa jina la Magauni Manne unaoendeshwa na Taasisi ya Maendeleo ya Vijana Mkoa wa Dodoma (DOYODO) .

Aliitaka jamii kuhakikisha wanawalinda watoto wa kike dhidi ya watu wenye nia mbaya ya kuwapa mimba wasichana wadogo na kukatisha ndoto zao za elimu na kimaisha .

"Na hapa nataka niseme, jamii nzima tuwalinde watoto wetu wa kike, kwa sababu wanaohusika kwenye hili ni vijana wetu na baadhi ya wababa wa hovyo wasio na huruma kuhusu maisha ya baadaye ya watoto wetu wa kike," alisema.

Kadhalika alisema serikali ilitunga sheria kali za kuwaadhibu wanaowapa mimba watoto wetu chini ya miaka 18 kwenda jela miaka 30, ili kuwalinda watoto wa kike dhidi ya mimba za utotoni.

Pia alisema elimu inayotolewa na vijana nchini na makundi mbalimbali imewasidia kulijenga kundi hilo na madhara wanayopata kutokana na kujihusisha na vitendo vya ngono katika umri mdogo .

Aliongeza kuwa serikali imeendelea kuboresha huduma za afya nchini kwa kujenga hospitali na vituo vya afya, ili kuhakikisha kila kundi linapata huduma hiyo muhimu .

Mkurungenzi Mtendaji wa DOYODO, Rajabu Nhunga, alisema mradi huo ulianza mwaka 2019 kwa lengo la kuwajengea vijana wa kike na kiume elimu ya maisha pamoja na kuzuia mimba za utotoni na umefikia mwisho, julai mwaka huu.

Nhunga alisema thamani ya mradi mzima ilikuwa dola za kimarekani 70,000 na ulikuwa ukitekelezwa katika Kata Tatu za Jiji la Dodoma, ambazo ni Chang'ombe, Miyuji na Nzuguni .

Alibainisha kuwa kutokana na fedha hizo waliweza kutoa elimu kwa makundi ya vijana wanaosoma shule ya msingi na sekondari pamoja na wale waliopo vyuoni na mitaani . Pia alisema mradi huo uliwashirikisha wadau wengine, ambao ni kutoka dawati la jinsia la Jeshi la Polisi, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Vijana, watendaji wa kata na mitaa, vijana, waalimu na watoa elimu rika.

Alibainisha kuwa mradi huo umeleta mafanikio kutokana na kuunda klabu za kutoa elimu hiyo ya kuzuia mimba za utotoni kwenye baadhi ya shule za msingi na sekondari

Aliongeza kuwa pamoja na mradi huo kufikia mwisho wanaendelea na jitihada za kutafuta wafadhili, ili kuendelea kutoa elimu hiyo kwenye maeneo mengine mkoa huo na mingine.




Mkurugenzi wa Taasisi ya Maendeleo ya Vijana Mkoa wa Dodoma (DOYODO), Rajabu Nhanga, akitoa taarifa ya utekelezaji wa kampeni ya kuzuia mimba za utotoni ijulikanayo kama "magauni manne" wakati wa hafla ya kufunga mradi huo, jijini Dodoma juzi, ambapo umefanikisha kutoa elimu hiyo kwa makundi mbalimbali ya kupambana na tatizo la mimba za utotoni. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Chamuriho apigia debe wahandisi wazawa, vijana kujengewa uwezo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhandisi Leonard Chamriho, ameiagiza Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB) kuhakikisha zabuni wanazozitoa zinakuwa na kipengele chenye takwa la kisheria la kuwajengea uwezo wahandisi wazawa hususani vijana.

Pia amesema katika mwaka wa fedha 2021/22 serikali imetenga Sh. trilioni 13.3, ambazo ni asilimia 37 ya Bajeti ya Taifa, kwa ajili ya kukamilisha miradi mbalimbali ya maendeleo nchini.

Chamriho alibainisha hayo juzi wakati akifungua maadhimisho ya 18 ya Siku ya Wahandisi (AED), kwa mwaka 2021.

Alisema lazima kipengele hicho kiwekwe na kiwe takwa la kisheria na isiwe hiari katika zabuni zote mpya za ujenzi, ili wahandisi wazawa, hususan vijana, wajengewe uwezo na ujuzi kubaki ndani ya nchi.

"Ujuzi huo wakiupata utabaki nchini na utawawezesha wahandisi wetu kuwa na uwezo mkubwa katika kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo hapa nchini, hivyo nawaagiza mhakikishe zabuni zote mpya mtakazoingia na kuzitoa kwa wakandarasi kigezo cha kujenga uwezo kiwe cha kisheria" alisisitiza

Pia alisema serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan, ilielekeza fedha zitengwe, ili kuwezesha miradai mikubwa yote iliyoanza kutekelezwa kukamilika na ambayo ilikuwa haijaanza ikamilike.

Kuhusu utekelezaji wa miradi kwa 'Force Account' ambao umekuwa ukisababisha makandarasi binafsi kukosa kazi, alisema serikali imeiona na tayari imeanza kuifanyia kazi kero hiyo kama alivyoelekeza Waziri Mkuu Kassim Majaliwa.

Msajili wa ERB, Mhandisi Patrick Barozi, alisema mpaka sasa bodi imesajili wahandisi 31,729 wanawake wakiwa 544 sawa na asilimia 32 na kuendeleza wahandisi 9,441 kati yao wanawake 756 kupitia mpango wao wa kuendeleza wahandisi nchini, ambao wamesajiliwa kwenye bodi hiyo kwa mwaka 2020.

Mwenyekiti wa Bodi ya ERB, Prof. Ninatubu Lema, aliwataka wahandisi kwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia na kujiandaa kukabiliana nayo katika utendaji kazi zao.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Antony Mtaka, alisema bado kuna shida katika utekelezaji wa miradi mbalimbali inayofanywa na wakandarasi wazawa huku akiwataka wanaoshinda zabuni kujenga uaminifu, ili kuaminika zaidi na kupewa kazi.





# Mwinyi awapongeza madaktari toka China

**Na Rahma Suleiman,** PEMBA

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, amefanya ziara ya kushtukiza katika Hospitali ya Abdallah Mzee iliyoko mkoani Pemba na kuwapongeza madaktari wa kutoka China waliojitolea kufanya kazi hapo ambao wamemaliza muda wao.

Akizungumza jana hospitalini hapo, alisema kuna kasoro nyingi katika hudima ikiwamo uhaba wa vitendea kazi na wafanyakazi.

Dk. Mwinyi alisema changamoto ya wafayakazi karibu itapatiwa ufumbuzi kwa kuwa anatarajia kufungua ajira kwa baadhi ya kada

Hata hivyo, alitaka uhakiki ufanyike vizuri ili kulipa madeni ya wafanyakazi na wahusika kuhakikisha madeni yanayohakikiwa hakuna madeni feki na kuwataka wafanyakazi kuendelea kujituma na kutoa huduma bora kwa wananchi na serikali itazifanyia kazi changamoto zilizopo

Awali, hospitalini hapo, madaktari walieleza changamoto iliyopo ni uhaba wa wafanyakazi na mrundikano wa posho zao.

Katika hatua nyingine, Rais Mwinyi alizindua boti za usafiri kwa ajili ya wananchi wa vijiji vya Kisiwapanza na Makongwe mkoa wa Kusini Pemba. Uzinduzi huo ulifanyika katika Bandari ya Mkoani.

Alisema boti hizo mbili zitasaidia kuwa na usafiri wa uhakika badala ya kutumia usafiri usiouhakika ambao unaweza kuhatarisha maisha yao.

Pia aliitaka mamlaka ya bandari kusimamia mapato ili kuboresha miundombinu katika bandari ya Mkoani Pemba likiwamo jengo la kufikia abiria.

Akifungua jengo jipya la Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) kwa upande wa Pemba, Rais Dk. Mwinyi alitoa onyo kali kwa wafanyabiashara wanaopandisha bei za bidhaa na kuwataka waache mara moja.

Licha ya kukiri kuwa bidhaa zinazotoka nje ya nchi kupanda bei kwa sababu ya changamoto za usafirishaji na ugonjwa wa corona, baadhi yao wametumia mwanya huo kupandisha bei za bidhaa zinazotoka ndani.

Alisema ujenzi wa jengo hilo lenye vifaa vya kisasa, uendane na mipango ya serikali ya kupandisha mapato kisiwani humo ambapo inapanga kufikia makusanyo ya Sh. trilioni 1.5 kutoka Sh. milioni 800 bilioni kwa miaka mitano.

Alisema kisiwa cha Pemba ni eneo maalum la kimkakati katika uwekezaji, hivyo wananchi wanatakiwa kupewa elimu ya kutosha kuhusu umuhimu wa ulipaji kodi.

Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Juma Maliki, alisema jengo hilo lililoanza kujenga mwaka 2019 limegharimu Sh. bilioni 10.6 na litatumiwa na taasisi ZRB na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), huku likiwa limewekewa vifaa vya kisasa vitakavyowezesha kufanya kazi kwa ufanisi.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akipokea zawadi ya kuku na ndizi kutoka kwa mmoja ya wazee wa kijiji cha Mleteni, Kaskazini Pemba juzi, alipofika kusikiliza kero za huduma za jamii ikiwa ni eneo ambalo halijawahi kufikiwa na kiongozi yoyote wa kitaifa tokea 1964. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Hemed aahidi ushirikiano na Oman

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amesema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) itaendeleza uhusiano na ushirikiano wake na Oman kwa maslahi ya wananchi wa pande mbili.

Hemed alieleza hayo ofisini kwake, Vuga, alipokutana na Balozi Mdogo wa Oman, Said Alsinawi, alipofika kwa ajili ya kujitambulisha.

Alisema SMZ inathamini ushirikiano wa kihistoria uliopo kwa muda mrefu ambapo Oman imekuwa ikiunga mkongo Zanzibar kupitia sekta mbalimbali hasa kuimarisha elimu kwa wananchi wa Zanzibar.

Makamu wa Pili wa Rais alimweleza Balozi huyo anayefanyia kazi zake Zanzibar kuwa wakati umefika kwa nchi hiyo kuja kuwekeza Zanzibar ikizingatiwa kwa sasa Zanzibar imejikita kukuza uchumi wake kupitia sekta ya uchumi wa bluu.

Naye Balozi Alsinawi alisema Oman itaendelea kushirikiana na Zanzibar kutokana na uhusiano wake wa kidugu wa miaka mingi iliopita.

Alisema Oman tayari imeonyesha nia yake ya kuwekeza Zanzibar kupitia sekta mbalimbali na kwa sasa mipango hiyo iko katika mchakato.

Alisema ujio wa ndege yao ya Oman ikiwa imebeba abiria wengi kwa safari zake Zanzibar ni kielelezo tosha cha ushirikiano baina ya nchi mbili hizo.

# ZEC yashauriwa ushiriki wanawake

**Na Mwandishi Wetu**

TUME ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC), imeshauriwa kushirikiana na Asasi za kiraia katika kufanya ushawishi kwa vyama vya siasa kuwashirikisha wanawake kugombea nafasi mbalimbali za uchaguzi

Ushauri huo ulitolewa jana na mjumbe kutoka Jukwaa la Mtandao wa Asasi za Kiraia, Hawra Shamte, wakati akiwasilisha mada ya utekelezaji wa sera ya jinsia na ushirikishwaji wa makundi maalum katika kikao kilichofanyika ofisi za ZEC, Maisara Mjini Zanzibar.

Hawra alisema ZEC ilianzisha sera ya jinsia na ushirikishwaji wa makundi maalum ya kijamii ya mwaka 2015 kwa lengo la kuhakikisha makundi yote ya kijamii, wakiwamo wanawake, vijana na watu wenye ulemavu wanashiriki katika hatua zote za uchaguzi ikiwamo kugombea katika uchaguzi.

Alisema jukwaa la mtandao wa asasi za kiraia ambalo limeundwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) upande wa Zanzibar, Jumuiya ya wanawake wenye ulemavu Zanzibar, Mtandao wa Vijana Zanzibar na Mtandao wa Asasi za Kiraia, limeipitia sera na kufanya utafiti wa utekelezaji wake kwa kipindi chote cha uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Naye Mkurugenzi wa TAMWA Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, aliipongeza ZEC kwa kuandaa sera nzuri yenye nia ya kuendesha uchaguzi unaowashirikisha wadau wa makundi maalum ya kijamii katika hatua zote za uchaguzi.

Mkurugenzi ya Rasilimali Watu, Mipango na Uendeshaji wa ZEC, Saadun Ahmed Khamis, aliwaomba wadau wa uchaguzi, vikiwamo vyama vya siasa na asasi za kiraia kuipitia sera hiyo na kuwasilisha changamoto ambazo zinajitokeza wakati wa utekelezaji wake.

Saaduni aliipongeza TAMWA kwa kuwa ni taasisi ya mwanzo kuipitia na kufanyia kazi sera ya jinsia na ushirikishwaji wa makundi maalum ya kijamii ya mwaka 2015 iliyotungwa na ZEC na kuwasilisha changamoto zao ambazo wameziona ni kikwanzo katika utekelezaji wake.



WHOZU

Uk.12





# HUYU NI SHILOLE? Mwonekano wazidi kutia shaka



MWILI wa mwanamuziki wa Bongo Fleva, Shilole, umezidi kujadiliwa na watu mbalimbali baada ya kuwa na wasiwasi kutokana na unene uliopitiliza.

Baadhi ya wasanii na mashabiki wa muziki kwa wiki sasa wamekuwa wakijadili umbo la mwanamuziki huyo, huku wengine wakimtaka kujiangalia upya kama anataka kuendelea katika muziki.

Katika kilele cha Wiki ya Wananchi, Shilole alipanda jukwaani akiwa amevaa jezi ya timu ya yanga, lakini mwonekano wake wa unene uliopitiliza uliwaacha watu wengi wakiwa katika mshangao.

Baada ya shoo yake hiyo, ndipo watu walipoanza kujadili na kwa maoni tofauti, kuna wale waliomtahadharisha kwa kueleza, lazima afikirie namna ya kupungua na baadhi walimuunga mkono kwa kusema ana haki ya kuwa anavyotaka.

Saidi Juma, amesema unene wa Shilole si jambo baya, lakini anaweza kupata matatizo kama hatachukua mazoezi ya kutosha kuufanya mwili kuwa imara.

"Unapokuwa mnene mwili unapambana na ongezeko la mafuta, ni lazima kupambana binafsi, ili kuufanya kuwa imara na kuweza kufanya kazi kama kawaida," amesema.

Aidha, ameonya kama anataka kuendelea na muziki ongezeko la mwili wake si jambo zuri kwani kuna wakati atashindwa kufanya kazi kama mashabiki wanavyotaka kutokana na kuelemewa na mwili.

Msanii mwenzake, Recho Kizunguzungu, naye amezungumzia hali hiyo kwa kueleza kwamba kunenepa au kupungua ni jinsi mtu mwenyewe anavyotaka.

"Kwenye suala la unene, kunenepa au kupungua ni mtu mwenyewe anavyotaka, Shilole anaishi na mume wake na mumewe ameridhika, mbona hajamwambia aende 'gym' au aende China akajipunguze, ameridhika na mwanamke wake"

# Poul Okoye aomba wamuache



MWANAMUZIKI wa Nigeria, Poul Okoye, amewashauri baadhi ya watu wanaoshabikia vurugu zinazotokea katika familia yake, waache kufurahia kwani suala hilo halina maana.

"Acheni familia yangu iwe na amani, ambayo tunaitafuta sasa, nawachukia wale wanazunguka na kusema kile wasichojua," amesema Okoye.

Paul na mkewe Anita wapo katika mgogoro mzito wa talaka huku akitaka kupewa kiasi cha dola 15,000, kama pesa za matunzo ya watoto wao.



## Kanye West kumbe kicheche pori

RAPA maarufu wa Marekani, Kanye West, amedaiwa kuwa na udanganyifu katika ndoa yake na kumfanya kutoaminika na mkewe Kim kardashian.

Kanye na Kim wametengana wakati maombi ya talaka yaliyofunguliwa na mkewe yakiendelea kujadiliwa.

Kulingana na mtandao wa Page Six, vyanzo vimefafanua kwamba katika moja ya nyimbo yake, Kanye alizungumzia jinsi alivyomtoroka mkewe na kwenda kujivinjari na mwanamke mwingine.

## Burna Boy tuone buti lako

MWANAMUZIKI Burna Boy, ameibua mjadala mkali baada ya kupanda jukwaani akiwa na kiatu cha aina yake, ambacho kiliwashangaza mashabiki wake.

Burna Boy, alikuwa na shoo yake siku ya Ijumaa huko uingereza katika ukumbi wa O2 Arena, wakati alipopanda jukwaani kuburudisha, watu walijikita kutazama kiatu hicho.

Kiatu hicho chenye rangi nyeusi kimetengenezwa na kampuni ya mavazi ya Rick Owens ya Marekani, ambayo inajihusisha na ubunifu, uzalishaji, usambazaji na uuzaji wa mavazi ambayo yamekuwa maarufu kutokana na upekee wake.





## BBNaija hakukaliki tena Tega, Boma walianzisha

WIKI hii shindano la Big Brother Nigeria, maarufu kama BBNaija, lilifikia patamu baada ya mume wa mshiriki kulalamika kusalitiwa na mkewe.

Malalamiko ya mume wa Tega ametoa malalamiko hayo, baada ya mkewe huyo kuanza uhusiano wa kimapenzi na mshiriki mwenzake Boma, ndani ya jumba hilo lililojaa kamera kila mahali.

Hata hivyo, mshiriki wa zamani wa BBNaija, Thelma, ameingilia mjadala huo kwa kusema Tega na Boma, wanafanya kitendo kisichofaa kwa kisingizio cha kupata umaarufu.

"Kwanza kabisa, huu ni ujinga wa mwanamke aliyeolewa. Niliona chapisho, ambapo mume alikuwa akithibitisha matendo yake, kwamba alimdanganya na ndio sababu anafanya hivi," Thelma aliandika kupitia ukurasa wake wa Instagram.

"Ingawa ninaelewa kuwa hii ni njia tu ya kuwafanya watu wamfuatilie, lakini onyesho hili peke yake ni sawa kabisa kwa mtu, ambaye anataka kuacha nyumba yake iteketee kwa makusudi," ameongeza.

## Iyanya ateuliwa msaidizi wa gavana

MSANII wa muziki mwenye mashabiki wengi Nigeria, Iyanya, sasa anatumikia cheo kipya cha kisiasa, ambacho kitamfanya ya kuwa mbali na jukwaa.

Kulingana na meneja wake wa zamani, Ubi Franklin, alitoa taarifa katika ukurasa wake wa Instagram, kwamba Iyanya ameteuliwa kuwa msaidizi maalum wa gavana wa jimbo la Cross River, Ben Ayade.

Baada ya taarifa hiyo, mashabiki walivamia ukurasa wake wakimpa pongezi na kumtakia kila la heri katika kazi yake hiyo mpya.



MAKALA

# UPOTEVU MAMILIONI YA TANI ZA SAMAKI

## •FAO, serikali zatua Kigoma kusaidia wavuvi Tanganyika

**Na Mwandishi Wetu**

WANANCHI wanaofanya shughuli za uvuvi katika ziwa Tanganyika hupoteza samaki kati ya asilimia 50 mpaka 70 kutokana na samaki hao kuharibika baada ya mavuno.

Uharibikaji huo unaanzia pale wanapovuliwa, kusafishwa, kuchakatwa, kukaushwa na hatimaye kufika sokoni ni kwa mujibu wa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya utafiti wa uvuvi nchini (TAFIRI), Dk Ismael Kimirei.

Anayasema hayo na kuongeza kuwa katika hali ya kawaida wavuvi wanaweza kupoteza samaki kati ya asilimia 40 na 50 lakini, wakati wa mawingu mazito na mvua za muda mrefu, wanaoharibika hufikia aslimia 70.

Anayasema hayo akizungumza katika Mradi wa FISH4ACP, kazi ya miaka mitano inayohusisha nchi 12 za Afrika, Caribbean na Pacific (nchi za ACP) na kwamba huo ni ushirikiano wa umoja wa nchi za Afrika, Caribbean na mataifa ya Pacific.

Dokta Kimirei, anaeleza kuwa wavuvi wengi katika Ziwa Tanganyika na kwingineko hupoteza samaki wengi kutokana na ukosefu wa vifaa na zana bora za kuvulia, kusafirisha, kuchakata, kuanika na kutunzia samaki waliowavua.

Anasema wavuvi wanapswa kujua kuwa baada ya kuvua samaki wanatakiwa kuwekwa na usafirishwa katika vyombo vyenye ubaridi mara moja, ambavyo havitasababisha samaki waharibike.

Anaeleza kuwa katika uchakataji, samaki wengi wamekuwa wakiharibika kutokana na muda mrefu unaopotea kabla ya kuwachakata, aidha zana duni zinatotumika kuchakata, pia husababisha samaki na dagaa wengi kuharibika.

"Baada ya kuvua, samaki wakichelewa tu kidogo huanza kutoa rangi fulani mfano wa sumukuvu, ambayo huharibu samaki kabisa kadiri muda unavyokwenda, anasema Dk. Kimirei,

Anatoa wito kwa wavuvi na wadau wengine kushirikiana na serikali katika kuhakikisha mradi huo wa kuongeza thamani na kuzuia upotevu wa samaki unatoa matokeo yanayokusudiwa.

Mmoja wa wachuuzi wa samaki katika soko la samaki la Kibilizi mkoani Kigoma, Majaliwa Matero, anasema ukosefu wa mitaji na mikopo ya bei nafuu vimechangia kufanya shughuli za uvuvi chini ya kiwango kutokana na kukosa vifaa vya kisasa.

"Tunaiomba serikali isaidie upatikanaji wa mitaji na mikopo, ili kuwawezesha wavuvi kuboresha vifaa vyao vya uvuvi kuanzia kuvua, kusafirisha, kuanika mpaka sokoni,"

Akizungumzia mikakati ya serikali, Mkurungezi wa viumbe maji (Aquaculture) katika Wizara ya Uvuvi Dk. Nazaeli Madalla, anasema serikali inalichukulia suala hilo kwa umuhimu wa hali ya juu.



Mchuuzi wa samaki wa soko la Kibilizi -Kigoma, Majaliwa Matero, akionyesha baadhi ya samaki wanaopatikana Ziwa Tanganyika. **PICHA: MWANDISHI WETU.**

"Kwanza inajaribu kuweka miundombinu bora na ya kisasa kuhakikisha upotevu na uharibifu wa samaki baada ya mavuno unapungua."

Anaongeza kuwa si rahisi kufanya hivyo mara moja, lakini kila mwaka serikali inatenga bajeti, kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu na wakati mwingine kuanzisha miundombinu mingine mipya.

"Jambo jingine tunalofanya kama serikali ni kuhamasisha wavuvi kuunda vikundi vya uvuvi, ili iwe rahisi kukopesheka. Pale wizarani tuna dawati linaloshughulika na sekta binafsi, ambalo lina jukumu la kuhamasisha, kuendeleza na kusaidia uundwaji wa vikundi hivyo vya wavuvi, wachakataji na wakulima wa samaki," anasema.

Anasema pindi wavuvi watakapo kuwa katika vikundi mbalimbali vya uvuvi, uchakataji na uzalishaji wanaweza kupata mikopo kwa urahisi kuendeleza shughuli zao za uvuvi.

"Kwa sasa tunajitahidi kuhakikisha kwamba tunawekeza katika mifumo baridi kuzuia upotevu na uharibifu wa samaki baada ya mavuno kwa kuweka miundombinu bora kama vile vifaa vya kupoozea, vyumba vya barafu na vyumba baridi, kuhakikisha kuwa hatupunguzi tu uharibifu wa samaki bali tunahitaji wavuvi watoe samaki wenye ubora," anasema.

Anasema samaki wanaanza kuharibika mara tu baada ya kutoka kwenye maji, lakini katika uvuvi bora unaofuata sheria na taratibu zote za uvuvi zinatakiwa kuwekwa kwenye mifumo na vyombo vyenye ubaridi au vyenye barafu, kuchakatwa na kupelekwa sokoni kwa walaji.

Anasema serikali inahamasisha pia ujenzi wa maeneo ya kuanikia. Pia inahamasisha uwekezaji katika vifaa hivi na kutaka wavuvi waondokane na mazoea ya kuanika samaki na dagaa chini kwenye mchanga, ili kuongeza ubora.

"Mvua ikinyesha ni matatizo kwa wavuvi maana hapo upotevu wa samaki baada ya mavuno unakuwa mkubwa mno, kwa sababu hakuna jua la kuwakausha. Ndiyo maana tunahamasisha na kuendeleza uwekezaji katika vyombo vinavyotumia umeme na sola, kwa ajili ya kukaushia samaki na dagaa. Tumeshaweka mifumo baridi katika mialo mbalimbali katika maziwa hapa nchini na huu ndiyo mwelekeo wa serikali kwa sasa.

Kadhalika aliongeza kuwa serikali inahamasisha na kuendeleza uanzishwaji wa viwanda vidogo, kwa ajili ya mnyororo wa thamani, ili bidhaa zetu ziweze kuuzwa ndani na nje ya nchi kwa ubora unaostahili.

Awali akielezea kuhusu mradi, Ofisa kutoka Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa (FAO), Hashim Muumin, anasema Mradi wa FISH4ACP ni wa miaka mitano unaohusisha nchi 12 za Afrika, Caribbean na Pacific, maarufu kama a ACP.

Anaongeza kuwa unafadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU) na Wizara ya Maendeleo ya Mashirikiano ya Uchumi ya Ujerumani na kutekelezwa na FAO.


Mradi unatumia na kujaribu njia zinazohusisha uchambuzi wa mnyororo wa thamani, ili kubaini na kuunga mkono uboreshaji wa mnyororo wa thamani na kuendeleza uvuvi na ufugaji na ukulima wa viumbe maji.

Tanzania imechaguliwa kuwa miongoni mwa nchi 12 zinazotekeleza mradi huu unaolenga kuongeza chakula na lishe na kulinda mazingira kwa maendeleo endelevu.

# KILIO UTUMWA WA NGONO

## •Ahadi elimu bora, tiketi bure zawaponza
## •Walazimishwa kulala wanaume 20 kila siku

**Na Mwandishi Wetu**



Hussain Ednanie na Shana Stanley walihukumiwa kwa kesi iliyohusisha wasichana wa Brazil

KAMERA zilizofichwa kwenye chumba cha kulala zimefichua vitendo vya kutisha vinavyofanywa na magenge ya kihalifu kwa kuwaweka utumwa wa kingono wasichana.

Katika kamera hizo zilionekana nyaraka kadhaa ikiwamo paspoti za wasichana hao pamoja na pesa.

Wasichana hao kutoka Brazil, walijikuta wakiwa katika kifungo cha nyumbani huku wakipigwa marufuku kuwasiliana na marafiki zao.

Wakiwa ndani ya nyumba hiyo, wanalazimishwa kushiriki ngono na wanaume 15 hadi 20 kila siku.

Maisha hayo yamekuwa ya kila siku kwa wasichana watatu kutoka Brazil, ambao hivi karibuni waliokolewa na polisi kutoka kwenye utumwa wa kingono huko North West London, nchini Uingereza.

Uchunguzi huo ulioanza Machi mwaka jana, ulihitimishwa mwezi Agosti 9, mwaka huu baada ya watuhumiwa Shana Stanley, mwenye miaka 29, na Hussain Edanie, (31), walipokiri makosa hayo .

Wote wawili wanakiri kufanya ngono na kuandaa safari kwa nia ya kunyanyasa wengine.

Waathirika wa vitendo hivyo ni wanawake watatu wa Brazil na mmoja kutoka Uingereza.

Edanie alihukumiwa kifungo cha miaka 8 na miezi miwili na Shana amefungwa miaka mitatu na miezi saba.

Chimbuko la kubainika kwa tukio hilo ni kutokana na uchunguzi wa BBC nchini Brazil ambayo ilionyesha hatari wanazokabiliana nazo watu wanaopewa ahadi za kirahisi za kusafiri na kupata ufadhili wa masomo nje ya nchi.

"Waliniuzia ndoto ambayo iligeuka kuwa jinamizi," anasema mmoja wa raia wa nchi hiyo ambaye bado anaendelea kupona msururu wa matukio ya unyanyasaji aliyokumbana nayo katika mji mkuu wa Uingereza.

**"Cheti chako cha kifo"**

Wabrazil hao watatu walifika Uingereza mwaka 2020, baada ya kupata ufadhili wa masomo wa kozi ya somo la Kiingereza ambayo ingedumu kwa wiki chache.

Hata hivyo, muda mfupi baada ya kuwasili, waligeuka kuwa wahanga wa soko lenye faida kubwa la usafirishaji haramu wa binadamu ambalo, kulingana na Umoja wa Mataifa, linaathiri watu milioni 2.5 kila mwaka.

Inakadiriwa biashara hiyo thamani yake ni zaidi ya dola bilioni 30 za Kimarekani.

"Shukrani kwa ujasiri na uhodari wa waathiriwa hao, tuliweza kukusanya ushahidi usioweza kukanushwa ambao ulimwacha Edani na Stanley bila chaguo lingine zaidi ya kukiri makosa yao ambayo yatazuia wengine kudhurika," anasema mpelelezi Peter Brewster, mmoja wa waliohusika na uchunguzi huo.

Yote hayo yalianza baada ya mmoja wa Wabrazil hao kuomba polisi msaada mnamo mwezi Machi mwaka jana, baada ya kuwepo ugomvi kati ya mwanamke aliyehukumiwa.

Wakati wanapigana, mwathirika alijaribu kuita polisi, lakini alisukumwa na Stanley, ambaye wakati huo, kulingana na rekodi rasmi, alimtishia kwa kumwambia kuwa aliweka mwenyewe sahihi kwenye cheti chake cha kifo.

Mwanamke huyo alizidi kuomba ulinzi wa polisi na kuonyesha picha za mnyanyasaji.

Katika ushahidi wake, mwathiriwa huyo alisema muda mfupi baada ya kuanza kozi yake ya somo la Kiingereza huko Manchester, alialikwa kusafiri kwenda London kukutana na mwanamke ambaye alikuwa amezungumza naye juu ya ufadhili wake wa masomo.

Baada ya kukutana naye, aliambiwa atalazimika kutia saini mkataba la sivyo hataweza kurudi Brazil na badala yake atalazimika kuishi mitaa ya London, kamwe hataweza kuiona familia yake tena.

Kulingana na polisi mkataba huo ulimtaka Mbrazili huyo auze mwili wake.

Aliwaambia wachunguzi kwamba hakuwa na njia mbadala na kwamba alisaini hati hiyo kwa kuhofia kutoweza kurudi Brazil.

Historia hiyo ilijirudia na Wabrazil wengine, ambao pia walikwenda Uingereza baada ya kuahidiwa ufadhili wa masomo ya Kiingereza, kupata malazi na tiketi za bure.

Katika kazi hiyo, watu hao walitaka kupata mapato ya dola 690 kwa siku.

Waathirika walipokea malipo ya kila wiki ya dola za 345, na dola 70 kwa ajili ya chakula.

Ili kufikia bei ya juu iliyoainishwa na wanyanyasaji, mara nyingi wanawake hao walilazimika kukutana na wateja 15 hadi 20 kwa siku moja, hiyo kwa mujibu wa polisi.

Kiasi kilichochukuliwa na walanguzi hao zingeweza kulipia gharama za kusafiri ambazo wasichana waliamini kuwa wamepata bure.

Katika vyumba vya kulala, kila kitu kilipigwa picha na kamera zilizodhibitiwa na wenzi hao.

Waliwaambia waathirika kuwa watatuma picha hizo kwa familia zao ikiwa hawatafanya kile walichoombwa.

Kiwango cha kuwahibiti wanawake hao kilikuwa cha juu zaidi.

Wasichana hao walipewa simu janja kutoka kwa walanguzi, ambazo walipata taarifa kuhusu ratiba za wateja kupitia mtandao wa WhatsApp na nyendo zao zote zilifuatiliwa kwa GPS.

Kwa muda mrefu, walilazimishwa kuongozana na mtu mwingine wakati wanaenda kufanya kozi yao ya Kiingereza, lakini walilazimika kuachana na masomo.

**SHERIA INASEMAJE**

Chini ya sheria ya Uingereza, ukahaba au kutoa huduma za ngono kwa ajili ya pesa ni shughuli ya kisheria.

Kwa upande mwingine, utekelezaji wa ukahaba kupitia takwimu maarufu kama 'pimps' na uwepo wa madanguro ni marufuku.

Polisi wa London wanasema "Tunachukua ripoti zote za utumwa wa kisasa kwa uzito mkubwa sana na wamejitolea kuwashtaki wale ambao wanahusika katika uhalifu huu mbaya,"

Wanasema pia wanahimiza mtu yeyote ambaye amepata uhalifu kama huo kuripoti haraka na kwamba malalamiko yao yatashughulikiwa kama suala la siri.

**WALIVYOPATIKANA NA HATIA**

Mnamo mwezi Aprili, mwaka 2020, polisi walitoa hati za kufanya msako dhidi ya anwani za watu hao waliowaleta Wabrazili hao na kukamata simu, nyaraka, orodha za bei na masanduku ya kondomu.

Maelfu ya pauni yaligunduliwa katika amana za pesa kwenye akaunti za benki za watu hao.

Ilikuwa baada ya upekuzi huu ndipo wachunguzi waliweza kumtambua mwathirika mwingine Mwingereza, mwanamke ambaye alisema alitafutwa na maajenti wanaoshughulika na wanamitindo.

Baada ya kupokea zawadi na kulipwa gharama zote na walanguzi hao walimlazimisha alipe deni na akawa hana budi zaidi ya kukubali kufanya kazi ya ukahaba.

Edani na Stanley waliwashawishi waathirika na ahadi za uwongo za kuwadanganya na kuwatumia kwa faida zao binafsi.

"Hawakuwa na heshima kabisa kwa waathiriwa au hata kujali ustawi wao, kiasi cha hata kuwalazimisha kufanya kazi kwa saa nyingi kuliko walivyokubaliana kwa malipo kidogo sana, hata wakati hawakuwa wanahisi wanaumwa." Brewster.

# Bunge: Bodi zote mashirika ya umma ziwe na wahasibu

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

BUNGE limeishauri serikali kuhakikisha bodi zote za wakurugenzi za mashirika yote ya umma zinakuwa na angalau mhasibu mmoja, ili kulinda mali ya umma.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Naghenjwa Kaboyoka, alitoa rai hiyo alipowasilisha bungeni jijini Dodoma jana, maoni ya ushauri wa kamati hiyo kuhusu kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu wa Mwaka 2021.

Alisema kamati yao inaishauri serikali kuzingatia suala hilo, ili walau kuwa na mhasibu mmoja, ambaye atakuwa msaada kwa bodi wanapojadili masuala ya usimamizi wa fedha.

"Ni vema Bodi zote za Wakurugenzi za mashirika yote ya umma kuwa na angalau mhasibu mmoja ambaye atasaidia kutoa ushauri kuhusiana na masuala ya usimamizi wa fedha," Naghenjwa aliwasilisha.

Mwenyekiti huyo pia alisema inapotokea serikali inakusudia kuwasilisha muswada bungeni, endapo sheria ina vifungu vingi ambavyo vinakusudiwa kufanyiwa marekebisho kwa wakati mmoja, ni vyema serikali ikatumia utaratibu wa kuifuta na kuiandika upya sheria hiyo.

Alisema utaratibu huo utaliwezesha Bunge kuifanyia kazi sheria hiyo kwa ufanisi zaidi kulinganishwa na inapowasilishwa kwa utaratibu wa marekebisho.

Naghenjwa alisema kamati yao inaona kuna umuhimu wa kutenganisha majukumu ya taasisi inayohusika na udhibiti wa sekta au taaluma na ile inayohusika na wanachama kwa kuunda chombo cha usimamizi (Public Oversight Body).

"Muswada haujaweka masharti kuhusu usimamizi wa wakaguzi wanaofanya kazi chini ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Suala hili liangaliwe kwa kina," alishauri.

Pia alisema PA inaona kuna haja uanzishwe mkakati mahsusi wa kupitia sheria zote zinazohusiana na taaluma mbalimbali nchini, ili kujiridhisha kama maslahi ya umma yamezingatiwa ipasavyo katika sheria hizo.

Vilevile, alisema serikali inapaswa kuweka utaratibu wa wanachama wa Chama cha Wahasibu Tanzania Bara (TAA) na Chama cha Wahasibu Zanzibar (ZAA), kufanya kazi kwa pamoja.

Naghenjwa alisema kamati imefanya uchambuzi wa maudhui ya marekebisho ya sheria hiyo na kubaini vikwazo vitatu ikiwamo wakaguzi wa hesabu kuandaa seti tofauti za taarifa za hesabu za fedha kwa nia ya kupotosha usahihi wa taarifa hizo.

Viwango vidogo vya adhabu vilivyopo kwenye sheria ya sasa kulinganishwa na uzito wa kosa, hali inayochangia ukiukwaji wa miongozo ya uandaaji wa hesabu.

Alikitaja kikwazo cha tatu kuwa ni kutokuwapo kwa masharti kwa wakaguzi wa hesabu kuwasilisha taarifa za ukaguzi Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA) na hivyo kusababisha kukosekana kwa kanzi data ya taarifa za hesabu.

# Wananchi watakiwa kuchangia maendeleo

**Na Costantino Michael,** TUDARCO

WANANCHI wametakiwa kutambua umuhimu wa kuchangia shughuli za maendeleo ili kuchochea maendeleo ya mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Wito huo umetolewa hivi karibuni na Ofisa Ufuatiliaji na Usimamizi wa Miradi wa Taasisi ya Maendeleo ya Jamii (CDTF), Suleiman Mpendo, wakati akizungumza na gazeti hili.

Alisema wamegundua kuna mwamko mdogo wa wananchi kuchangia shughuli za maendeleo wakiwa na dhana ya kuwa maendeleo yanaletwa na serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO).

"Jamii inapaswa itambue kuwa wao ndiyo msingi na nguzo ya kuleta maendeleo katika maeneo yao, hivyo wana wajibu mkubwa wa kujitoa na kuchangia shughuli za maendeleo ipasavyo.

"Kwa mfano kama kuna mradi wa ujenzi unaotekelezwa wanajamii wanapaswa kushiriki kubeba vifaa vya ujenzi na kuchangia nguvu kazi kwa kufanya kazi za mikono, lakini kinachoshangaza utakuta wananchi hawajitokezi kufanya kazi hizo na wanaawaachia viongozi wa serikali na wadau wa maendeleo wanaosaidia utekelezaji kutekeleza wenyewe miradi inayoanzisha," alisema.

Kwa mujibu wa Mpendo, utafiti nchini umeonuesha kuwapo kwa hamasa ndogo ya wananchi kuchangia shughuli za maendeleo.

"CDTF tumegundua kuna baadhi ya wadau wa maendeleo wanaotekeleza miradi kwenye halmashauri zetu hawawashirikishi wananchi hivyo kuibua malalamiko yanayosababisha ushiriki mdogo,"alisema.


## CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA SERIKALI ZA MITAA TANZANIA TALGWU

## TANGAZO LA NAFASI ZA AJIRA

Katibu Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (TALGWU) anawatangazia nafasi za Ajira kama ifuatavyo:-

**1.0 KATIBU WA MKOA DARAJA LA II TGRS D (Nafasi 3)**

**1.1 Sifa na uzoefu**

i. Kuajiriwa mwenye shahada ya kwanza katika fani ya sheria, utawala, sosholojia, mipango au Elimu kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali.
ii. Awe na ufahamu wa matumizi ya kompyuta
iii. Awe na umri usiozidi miaka 45
iv. Mwanachama wa TALGWU atapewa kipau mbele

**1.2 Kazi za kufanya**

i. Mwakilishi wa Katibu Mkuu katika Mkoa husika
ii. Atakuwa ndiye msemaji Mkuu wa Chama katika Mkoa
iii. Kuratibu na kutatua Migogoro kati ya Mwajiri na Mwanachama wa TALGWU ambayo imeshindikana kupata ufumbuzi.
iv. Kumsaidia Katibu Mkuu katika kufanya majadiliano ya Hali Bora kwa Wanachama katika Halmashauri za Mkoa husika
v. Kuandaa mapendekezo ya Bajeti ya Mkoa na kuiwasilisha kwa Katibu Mkuu kwa ajili ya kuunganishwa katika Bajeti ya Chama
vi. Kuratibu zoezi zima la kuandikisha Wanachama wapya kutoka katika Halmashauri za Mkoa wake na taasisi nyinginezo.
vii. Kusaidia kuratibu na kutoa mafunzo kwa Wanachama katika Mkoa kwa kushirikiana na Idara za kuratibu mafunzo katika Chama
viii. Kuratibu shughuli za uanzishwaji wa Mabaraza ya Wafanyakaz na kuhakikisha kwamba yanafanya kazi wakati wote
ix. Kuwa Katibu wa vikao vyote vya Chama katika Mkoa
x. Kuandaa taarifa za kazi na fedha za Chama katika Mkoa

**2.0 AFISA MANUNUZI DARAJA LA II TLGS D (Nafasi 1)**

**2.1 Sifa na uzoefu**

i. Kuajiriwa mwenye Shahada ya kwanza katika fani ya Manunuzi au Ugavi kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali
ii. Awe na cheti kutoka katika Bodi ya Manunuzi
iii. Mwenye uzoefu wa kufanya kazi za Manunuzi atapewa kipaumbele zaidi
iv. Mwanachama wa TALGWU atapewa kipau mbele
v. Awe na umri usiozidi miaka 45

**2.2 Kazi za kufanya.**

i. Kukusanya takwimu za kusaidia kutayarishwa makisio ya vifaa vinavyohitajika na Mpango wa Ununuzi (procurement plan)
ii. Kukusanya na kutunza takwimu za Wazabuni mbalimbali katika Chama
iii. Kukusanya na kutunza takwimu za upokeaji, utunzaji na usambazaji vifaa
iv. Kubuni mfumo mzuri wa uwekaji na utunzaji wa vifaa
v. Kusimamia ukaguzi wa kihesabu wa vifaa vya Chama mara kwa mara
vi. Kusaidia katika shughuli za Miradi ya Chama
vii. Kutayarisha taarifa za kazi katika mwezi, Robo mwaka na kila mwaka
viii. Kuwa Katibu wa vikao vya Bodi ya zabuni katika Chama
ix. Kufanya kazi nyinginezo atakazopangiwa na Mwajiri wake

**3.0 MHASIBU MSAIDIZI DARAJA LA II TLGS C (Nafasi 2)**

**3.1 Sifa na uzoefu**

i. Kuajiriwa mwenye Stashahada ya kawaida katika fani ya Uhasibu kutoka katika chuo kinachotambuliwa na Serikali.
ii. Mwenye uzoefu wa kufanya kazi katika mamlaka za Serikali za Mitaa na Mwanachama wa TALGWU atafikiriwa zaidi

**3.2 Kazi za kufanya.**

i. Kupokea na kulipa fedha
ii. Kutunza daftari la fedha
iii. Kukagua hati za malipo
iv. Kufanya usuluhishi wa kibenki
v. Kufanya kazi nyinginezo kama atakavyopangiwa na mkuu wake wa kazi.

**4.0 MTUNZA KUMBUKUMBU MSAIDIZI II TLGS C (Nafasi 3)**

**4.1 Sifa na uzoefu**

i. Kuajiriwa watumishi wenye cheti cha kidato cha IV au VI na waliohudhuria mafunzo ya utunzaji wa kumbukumbu na kupata cheti cha NTA level 5 katika fani ya masjala na mahakama.

**4.2 Kazi za kufanya.**

i. Kupokea, kuchambua, kusajili na kuhifadhi kumbukumbu zote katika majalada na sehemu nyinginezo.
ii. Kutafuta kumbukumbu/ nyaraka na majalada na kuyapeleka kwenye ofisi husika
iii. Kuhifadhi kumbukumbu katika mpangilio mzuri na unadhifu
iv. Kuandika vitabu vya kufungulia majalada na nyaraka ili kurahisisha upatikanaji wa kumbukumbu
v. Kuhakikisha kwamba kumbukumbu zilizokwisha muda wake zinahifadhiwa vizuri au kuharibiwa katika mazingira salama.
vi. Kusimamia mzingo wa majalada (file movement)
vii. Kushauri na kusaidia katika kuandaa sera za uhifadhi wa kumbukumbu za Chama
viii. Kufanya kazi zingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi.

**5.0 KATIBU MAHSUSI DARAJA LA II TLGS C (Nafasi 2)**

**5.1 Sifa na uzoefu**

i. Kuajiriwa watumishi wa kidato cha IV /VI wenye cheti cha NTA level 6 kutoka katika chuo kinachotambuliwa na Serikali.

**5.2 Kazi za kufanya.**

i. Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida
ii. Kupokea wageni na kuwasaili shida zao na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa
iii. Kutunza kumbukumbu za matukio, tarehe za vikao, safari za mkuu wake na ratiba ya kazi zingine zilizopangwa kutekelezwa katika ofisi anamofanyia kazi na kumuarifu mkuu wake kwa wakati unaohitajika.
iv. Kusaidia kutafuta na kumpelekea mkuu wake majalada, nyaraka au kitu kinachohitajika katika shughuli za kazi.
v. Kupokea majalada, kuyagawa kwa maafisa walio sehemu alipo, kuyakusanya kuyatunza na kuyarudisha sehemu zinazohusika.

**6.0 DEREVA DARAJA LA II TLGS B (Nafasi 1)**

**6.1 Sifa na uzoefu**

i. Kuajiriwa wenye cheti cha mtihani wa kidato cha IV, wenye leseni daraja la "C" ya uendeshaji wa magari pamoja na uzoefu wa kuendesha magari kwa muda usiopungua miaka miwili bila kusababisha ajali, wenye cheti cha majaribio ya ufundi daraja la II kutoka Chuo cha usafirishaji (NIT).

**6.2 Kazi za kufanya.**

i. Kuendesha magari ya ofisi
ii. Kuhakikisha gari na vyombo vyake vipo katika hali nzuri wakati wote na kufanya uchunguzi wa gari kabla na baada ya safari ili kugundua ubovu unaohitaji matengenezo
iii. Kutunza na kuandika daftari la safari ("log book") kwa safari zote
iv. Kufanya majukumu mengine kama atakavyopangiwa na mkuu wake wa kazi

**7.0 NAMNA YA KUTUMA MAOMBI**

Waombaji wenye sifa zilizotajwa watume maombi yao kwa:

**Katibu Mkuu**
**Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (TALGWU)**
**S.L.P 16097**
**DAR ES SALAAM**

**NB:** Barua zote za maombi ni lazima ziambatanishwe na Wasifu (CV) wa muombaji, picha moja "passport size" ya hivi karibuni. Na nakala zilizothibitishwa za viwango vya ufaulu na vyeti vya taaluma. Majina matatu ya Wadhamini yaonyeshe anuani nan amba zao za simu. Maombi yatumwe kwa njia ya posta.

Pia Tangazo hili linapatikana kwenye Tovuti ya TALGWU **www.talgwu.or.tz**

Mwisho wa kutuma maombi ni siku kumi nan ne (14) tangu tarehe ya tangazo hili.

Rashid M. Mtima
KATIBU MKUU – TALGWU TAIFA


# MATANGAZO MCHANGANYIKO


**MATANGAZO MCHANGANYIKO**

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU** KUTOKA ENTEPRISES FINANCE LIMITED (EFL). KWA MAWASILIANO ZAIDI **TUPIGIE:0677 111 333 AU 0758 112 332**

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**


## KUPOTEA KWA CHETI



**JULIUS D MACHILIKA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1862/0082** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary MESAC mwaka 2017,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **DAR/CEN/RB/423079/2021**

116441402

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**HERI ENOCK EMMANUELI** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA IST YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 337 CWB** YENYE CHASSIS **NO.NCP650011466** NA ENGINE NO **1NZ2510866** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI **KAH/ RB/448/2021**

116440502

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

Ndugu **BERTAM BENEDICT MINDE** anatangaza kupotelewa kwa kadi yake ya gari aina yake SUZUKI(ESCUDO) yenye usajili namba **T 192 APS** Kwa yeyote atakae ona au kuokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Rb Namba. **MOR/MOR/RB/420770/2021**

116440102

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**PASCAL M .KIHWELO** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA **LANDROVER** YENYE NAMBA ZA USAJILI **T779AGP** LENYE CHASES NAMBA **SALLHAME8EA321875** INJINI NAMBA **9001011913** MALI YA DIOCESE YA IRINGA KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA POLISI TAARIFA YA POLISI RB. NAMBA **IRI/IRI/RB/431267/2021**

116441702

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**PASCAL M .KIHWELO** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA **LANDROVER** YENYE NAMBA ZA USAJILI **T381AGP** KADI NAMBA **331029** LENYE CHASES NAMBA **123050** INJINI NAMBA **90297216** MALI YA DIOCESE YA IRINGA KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA POLISI TAARIFA YA POLISI RB.NAMBA **IRI/IRI/RB/431264/2021**

116441802

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**GLORIA NOVATUS MUSHI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA ALLION** yenye namba za usajili **T 347 DKF** chasis namba **ZZT240-0011425** engine namba **1ZZ 0965645,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **DAR/SEL/RB/431289/2021**

116441201

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika Mahakama ya Mwanzo MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi NO.273/2021**

**Ombi la FATMA RAJAB HASSAN Kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu RAJAB HASSAN MADEBE**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe 22/09/2021 kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 02/09/2021

MAHAKAMA YA MWANZO MJINI MOROGORO

116440302

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**IN THE DISTRICT REGISTRY OF BUKOBA, AT BUKOBA**

**LAND CASE APPEAL 100/2020**

**FAUDHA AHAMADI**
**(Administratrix of the estate of the late**
**HAMADI ISMAIL DAUDA) ......................................APPELLANT**

**VERSUS**

**FATUMA ISMAIL ..............................1st RESPONDENT**
**JACKEM AUCTION MART BROKER LTD ..........2nd RESPONDENT**

**TO; JACKEM AUCTION MART BROKER LTD**

**RE: NOTICE FOR DATE OF MENTION**

Whereas the above mentioned applicant has lodged a case registered as Land Case Appeal no. 3/2021 against you at the High Court of Tanzania at Bukoba 4th day of October, 2021 at 09:00 am before Hon. A MWIPOPO J. You are required to appear in person or through your Advocate.
Take further notice that in default of your appearance on that date and time for the said mention the case will proceed in your absence.
Given under my hand and seal of the court this 26th day of August, 2021.

**J. M. MINDE**
**DEPUTY REGISTRAR**
**HIGH COURT OF TANZANIA**
**BUKOBA**

116441502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya njombe**

**Kituo cha njombe mjini Mkoa wa njombe**

**Usimamizi wa mirathi na 48/2017**

**Joseph simon mwaluanda.......marehemu**

**Kelvin joseph mwaluanda.....mwombaji**

**TAARIFA KWA UMMA**

**MAOMBI YA KUTANGAZA KUFUNGA MIRATHI**

Kwa wote wanaodai kuwa na haki na marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia orodha ya mali za marehemu na hesabu za mirathi katika jalada la mirathi
Mapingamizi yoyote kuhusu orodha ya mali na au hesabu za mirathi hii yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya siku ya tarehe 19 ya mwezi septemba mwaka 2021
Imetolewa na hakimu mkazi leo siku ya tarehe 19th agosti mwaka 2021

HAKIMU MKAZI

116440402

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.... OF 2021**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE**
**ELISHA WILSON MALEBETO**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION**
**BY EMANUEL ELISHA WILSON**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the **24 day of SEPTEMBER 2021.**

**Dated at Dodoma this 21 day of JULY 2021**

116440202


**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HADITHI

TOM alipooa alidhani kuwa ataishi kwa amani, furaha na kupata utulivu kama inavyokuwa kwa rafiki na wenzake wote waliofanya hivyo.
Siku zote ndoa ni masikilizano, maelewano, na anayeoa hupata furaha na heshima. Kinyume chake, kwake amekuwa ni misukosuko, mikosi na balaa. Badala ya kuwa ndoa yenye furaha, akajiingiza kwenye mtego hatari ambao hata baada ya kuufahamu, hakuweza kuutegua tena. Alichelewa. Ukawa ni mwanzo ni vilio, maafa na mtiririko wa mambo ya kushangaza.
Hebu pata kila nakala ya gazeti hili kufuatilia kisa hiki cha kushangaza na kusikitisha.

# Namsaka Mke Wangu-10

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Alikuwa hajaelewa kuwa ni kweli Tom ataondoka naye, au anamtumia, lakini akimaliza atatoroka, na huenda akamdhuru Sam na kumrudia mkewe Farida.

Pamoja na yote aliamua kujaribu bahati yake.

"Kama ikishindikana akinitoroka na mimi nitatoroka na kurudi kwetu Manyoni." Alijiambia.

"Kumbuka, ukimuwekea hiyo dawa, usichukue kila kitu. Tafuta vitu ambavyo vinaweza kunisaidia mimi kupata ninachokihitaji. Na hiyo itakuwa ndiyo salama ya kutokukugusa. Nadhani nimeshakwambia kila kitu. Kilakinachonihusu na mke wangu unakijua. Tena nimekumbuka, hata simu yake chukua, halafu tutajua baadaye."

"He baba, sawa, ila umenipa mzigo mzito, maana mimi umenifanya sasa kama polisi mpelelezi."

"Ndiyo utaanza karatibu kujifunza."

"Enhee, kitu gani cha kwanza kinatakiwa?"

"Twende mjini kwanza. Nikakununie nguo nzuri za gharama. Halafu tupitia saluni, usuke mtindo ambao wewe ukisuka unakupendeza sana. Yaani leo jioni uwe kama malaika. Akikuona atababaika. Ila la muhimu. Akisema twende nyumba ya wageni, kataa kwa sabbu huko hatutopata kitu tunachohitaji, hata kama utamuwekea dawa."

"Nimekuelewa hani. Leo kwa Mwenda watanikoma, naingia siyo baamedi tena. Naingia kama msichana mrembo nitakayetetemesha baa nzima." Alijigamba na baadaye akauliza "Wewe nawe vipi?"

"Mimi nitarudi kwenye sura yangu ile ulioiona mara ya kwanza."

*****************************

Kila kitu kilienda kama kilivyopangwa. Siku iliwadia. Shopingi ilifanywa. Tedi alipelekwa saluni. Akapambwa akapambika. Akavaa akang'aa. Tom naye hakuwa nyuma. Alipiga pamba zake ambazo alidhani kuwa zingempendeza. Kiasi alipendeza. Kila aliyemtazama mwenzake alicheka. Akampongeza kuwa amependeza.

Waliongea mengi. Wakafanya mengi. Lakini kila mmoja alikuwa na lake moyoni alilofikiria. Ni kuhusu kazi wanayokwenda kuifanya. Na haswa Tedi. Kwake ilikuwa ni kazi ngumu. Ni kwa vile mtu aliyemtuma kwa siku




**"Leo inaweza kuwa vizuri zaidi kwa sababu hana mwanamke, anaweza kunitongoza akataka niende naye." Tedi**

chache tu ambazo amekaa naye aligundua kuwa ni mtu mzuri. Mkarimu. Mcheshi na mwenye huruma. Ni tofauti na mwanzo alivyofikiria. Alianza kumshangaa mwanamke mwenzake Farida kumtoroka mwanaume wa aina hiyo wiki moja tu baada ya ndoa. Awali alidhani kuwa huenda ni mwanamke katili, mnyanyasaji.

Pamoja na hayo aliwaza kuwa kuna baadhi ya wanaume huficha makucha yao wanapopata wanawake wapya. Au mwanzoni mwa mapenzi. Baadaye wanakuja kuonyesha tabia yao halisi.

Licha ya yote hakutaka kumpoteza. Tayari walishapanga mipango mingi, ikiwemo kumlipia ada ya shule ya urembo. Hilo alikuwa na uhakika nalo. Yaliyobaki alimuachia Mungu.

Waliingia kwenye baa ya Mwenda. Macho ya watu wengi yalikuwa kwake. Kila mmoja alimshangaa Tedi.

Tedi huyu huyu ambaye ni baamedi kwenye baa ile. Hakuwa Tedi yule tena wanayemfahamu. Kwa siku chache amekuwa adimu kwenye baa hiyo. Awali alipoingia si wengi waliomfahamu.

Pamoja na kwamba Tedi ni msichana mrembo, lakini ulizidi kwa siku chache baada ya kuwa na Tom.

Tom hakumuacha kurudi tena kufanya kazi yake ya zamani. Alimtumia kwa kampani. Pamoja na kazi nyingine ambayo amempa kuifanya.

Hata baadhi ya wenzake, ikiwemo yule ambaye alimfanyia mipango kuwa na Tom walianza kumuonea wivu. Walijua ni msichana mzuri. Lakini hawakuwahi kufikiri kuwa kumbe Tedi ni mrembo zaidi kuliko walivyodhani.

Walikwenda kuketi kwenye siti ambayo ilikaribia siku ile ya kwanza walipokaa. Wakaagiza vinywaji. Walianza kunywa kwa furaha kama mtu na mpenzi wake. Ilikuwa ni zaidi ya siku ile ya kwanza. Sasa hivi wameshazoena.

Robo saa baadaye Sam aliingia. Tom na Tedi mawazo yake walijua kuwa angeambatana na Farida kama ilivyokuwa siku ile au zingine nyuma. Haikuwa hivyo. Alikuwa peke yake. Wasiwasi wa kwenda na Farida ndiyo ulimfanya Tom kubadili sura yake kama anavyofanya siku zote.

Kwa mbali alianza kuingia na furaha. Aliona kutokupo kwa mkewe Farida kungeweza kurahisisha kazi au mpango mkakati alioupanga.

"Leo inaweza kuwa vizuri zaidi kwa sababu hana mwanamke, anaweza kunitongoza akataka niende naye." Tedi alimnong'oneza Tom.

"Na ndiyo maana nifanya haya yote." Alijibu Tom na kuona mawazo yake yanafanana na Tedi.

"Kilichobaki toka hapa nenda kapite pale karibu yake, tembea kwa madaha kuelekea msalani hadi akuone, halafu tuone nini kitaendelea."

Tedi alinyanyuka. Kwa madaha ya kike alianza kupiga hatua moja kwa mpangilio maalum. Alipita mbele ya meza aliyokuwa amekalia Sam. Mwanaume ambaye ndiye anayeonekana kuongozana na Farida, mke wa Tom, aliyemtoroka wiki moja baada ya harusi.

"Tedi hakumchanganya Sam tu pekee. Wanaume wengi ndani ya baa walionekana kunyanyasika na urembo wa ghafla ya Tedi. Macho yote yalikuwa kwake.

Haikupita hata dakika moja, Sam alisimama. Alionekana kama kuna mtu anamtazama. Halafu akaanza kutembea kuelekea msalani. Kwa ramani ya baa ile, au baa nyingi nchini. Vyoo vya wanaume na wanawake wala haviwi mbali sana. Vinapenana migongo tu, au milango tofauti.

Alikoelekea Sam ni kule kule tu alikoelekea Tedi. Kwa jicho la tatu, Tom alijua Sam anamfuata Tedi. Anataka kumvizia akitoka msalani amwambie jambo. Hadi wakati huo alikuwa anafuahia mpango wake kuwa unaelekea vizuri.

Hakutaka kuangalia zaidi. Alijua Tedi atakuja kumweleza kila kitu kilichoendelea. Aliendelea kupiga kinywaji. Muda si muda Tedi alirejea na tabasamu mdomoni.

"Vipi, mbona umefurahi sana."

"Mhhh, rafiki yako huyo."

"Nani?"

"Sam. Si kanisimamisha. Akaniambia umempata buzi siku hizi anakupendezesha, basi sisi unatuona takakata."

Tom alicheka kicheko kifupi. "Yaani mimi nimeshakuwa buzi?"

"Anakwita buzi. Akanikumbushia siku ile nilikutongoza ukanitolea nje kwa sababu ya yule mwanamke, leo hayupo, unasemaje. Nikamwambia yaani nimuache bwana yangu pale niondoke na wewe, inawezekana kweli. Akaniambia hata kesho. Nikamuuliza yule mwanamke wako vipi? Akaniambia amekwenda Dar es Salaam kwa ndugu zake atarejea baada ya siku tatu kuanzia leo."

"Enhee halafu?"

"Nikamwambia basi tufanye kesho. Akaniomba namba ya simu nikampa. Lakini nikamwambia mimi masuala ya kunipeleka kwenye nyumba ya wageni sitaki. Kama unanihitaji basi iwe kwako. Na nikamdanganya kuwa kesho sitaki uwepo kwenye baa hii, twende kwingine kwa ajili ya kukukimbia wewe ili usitukute. Yote amekubali."

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

## HABARI MICHEZO

MECHI KALI
HOME
QATAR
7.03 | 5.23 | 1.38
PORTUGAL
AWAY
1 WEKA PESA.
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4 - WEKA PESA.
- FUNGUA MENYU YA HALOPESA
- CHAGUA LIPA/LIPIA BILI
- WEKA NAMBA YA KAMPUNI 150888, KUMBUKUMBU 888.
- KISHA WEKA 500 AU ZAIDI.
SEND
vodacom m-pesa airtel money tigo pesa EZYPESA halopesa
2 WEKA BET.
- PIGA *150*87#
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 468

# KANE AKERWA NA UBAGUZI WA MASHABIKI



**LONDON,** England

STRAIKA wa England, Harry Kane, ameshauri mamlaka ya soka kuwachukulia hatua kali mashabiki wa Hungary baada ya kuhusika kwenye ubaguzi wa rangi katika mchezo wa Alhamisi wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 4-0.


Baada ya Raheem Sterling kufunga bao la ufunguzi wakati akisherehekea alipigiwa kelele za kumfananisha na nyani, huku pia hali kama hiyo ilijitokeza wakati Jude Bellingham akiingia uwanjani.

"Nitazungumza na wachezaji kuona nini cha kufanya. Tutatakiwa kuripoti FIFA na ni matumaini yangu watachukua hatua kali."

UEFA iliwafungia mechi mbili mashabiki wa Hungary wakati wa michuano ya Ulaya kipindi cha majira ya joto kwa sababu ya ubaguzi wa rangi, lakini FIFA ilitengua adhabu hiyo na kuruhusu mashabiki kuingia uwanjani.

Naye kocha wa England, Gareth Southgate, aliwashutumu mashabiki wa Hungary kwa kuwazomea na kuwafananisha na nyani, Raheem Sterling na Jude Bellingham.

"Ilikuwa inakatisha tamaa kuona mashabki wakiwazomea wachezaji wetu, na ilishatokea kwenye mchezo uliopita, nafurahi kwamba vijana wangu walisimama pamoja katika hilo," alisema mlinzi wa kati, Harry Maguire akiiambia BBC Radio 5 Live.



# Pjanic apelekwa Besiktas kwa mkopo

**BARCELONA,** Hispania

KLABU ya Barcelona hatimaye imemtoa Miralem Pjanic, ambaye sasa amejiunga na klabu ya Besiktas kwa mkopo akitokea kwa miamba hao wa LaLiga, baada ya kuwa na msimu mmoja mbaya.

Pjanic aliwasili Camp Nou mwaka 2020 kwa ada iliyoripotiwa kuwa euro milioni 60 huku wakibadilishana na Arthur ambaye alikwenda Juventus kwa ada ya euro milioni 72.

Lakini tangu kutua hapo Barca, Pjanic hakuwa na kiwango cha kuvutia sana akipata nafasi chache za kucheza.

Pjanic alishindwa kupata namba mbele ya kijana Ilaix Moriba katika kipindi cha pili cha msimu wa 2020-21.

Pjanic alicheza mechi 30 kwenye mashindano yote, lakini alianza kwenye mechi 13, huku nne akitokea benchi baada ya kuwasili kwa kocha, Ronald Koeman.

Hakufunga bao lolote wala kutoa asisti kwenye mechi zote za mashindano, akijiwekea rekodi yake ya kucheza dakika 170 bila kufunga bao.

Taarifa ya Barca ilisema: "Barcelona na Besiktas wamefikia makubaliano ya kumpeleka kwa mkopo mchezaji, Miralem Pjanic ambapo atacheza huko hadi Juni 30, 2022.

## HABARI MICHEZO


,576,020

# JACKPOT

## MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 04/09/21 | 17:00 | Exeter vs Forest Green | 2.95 | 3.24 | 2.31 |
| 02. 04/09/21 | 17:00 | Carlisle vs Salford City | 2.65 | 2.95 | 2.75 |
| 03. 04/09/21 | 17:00 | Oldham vs Barrow | 2.45 | 3.19 | 2.79 |
| 04. 04/09/21 | 17:00 | Stevenage vs Swindon Town | 2.54 | 2.94 | 2.89 |
| 05. 04/09/21 | 17:00 | Newport vs Leyton Orient | 2.56 | 2.95 | 2.85 |
| 06. 04/09/21 | 17:00 | Colchester vs Sutton United | 2.38 | 3.03 | 3.03 |
| 07. 04/09/21 | 17:00 | Southend vs Wrexham | 2.54 | 3.22 | 2.63 |
| 08. 05/09/21 | 01:30 | Remo PA vs Botafogo RJ | 2.89 | 3.09 | 2.35 |
| 09. 05/09/21 | 03:00 | Bahia BA vs Fortaleza CE | 2.57 | 3.15 | 2.57 |
| 10. 05/09/21 | 03:00 | Cuiaba MT vs Santos | 2.36 | 3.11 | 2.86 |
| 11. 05/09/21 | 05:00 | San Jose Earthquake vs Colorado Rapids | 2.49 | 3.46 | 2.70 |
| 12. 05/09/21 | 19:15 | Mirandes vs Las Palmas UD | 2.62 | 2.81 | 2.96 |
| 13. 05/09/21 | 19:30 | Patronato Parana vs Talleres | 2.80 | 2.94 | 2.51 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMAMOSI - 04 - SEPTEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 2139 | Falkenbergs vs Akropolis IF | 1.95 | 3.54 | 3.79 |
| 16:00 | 4323 | Finland vs Kazakhstan | 1.43 | 4.28 | 7.76 |
| 16:00 | 5479 | IK Brage vs Landskrona Bois | 2.95 | 3.40 | 2.34 |
| 17:00 | 1674 | Cliftonville Belfast vs Glentoran Belfast | 3.29 | 3.43 | 2.00 |
| 17:00 | 1775 | Mansfield vs Harrogate | 1.87 | 3.44 | 3.93 |
| 17:00 | 2132 | Operario PR vs Vitoria BA | 2.03 | 3.05 | 3.63 |
| 17:00 | 2414 | Bristol Rovers vs Crawley Town | 2.00 | 3.43 | 3.48 |
| 17:00 | 2558 | Carlisle vs Salford City | 2.65 | 2.95 | 2.75 |
| 17:00 | 2849 | Exeter vs Forest Green | 2.84 | 3.23 | 2.39 |
| 17:00 | 3025 | Tranmere vs Hartlepool | 2.51 | 3.15 | 2.75 |
| 17:00 | 3392 | Stevenage vs Swindon Town | 2.54 | 2.94 | 2.89 |
| 17:00 | 3907 | Cheltenham vs MK Dons | 2.50 | 3.14 | 2.80 |
| 17:00 | 3963 | Accrington vs Shrewsbury | 2.08 | 3.16 | 3.60 |
| 17:00 | 4022 | Northampton vs Scunthorpe | 1.82 | 3.34 | 4.33 |
| 17:00 | 4072 | Newport vs Leyton Orient | 2.43 | 3.10 | 2.90 |
| 17:00 | 4155 | Colchester vs Sutton United | 2.46 | 2.90 | 3.05 |
| 17:00 | 4326 | AFC Wimbledon vs Oxford Utd | 2.95 | 3.49 | 2.22 |
| 17:00 | 4640 | Port Vale vs Rochdale | 2.15 | 3.23 | 3.28 |
| 17:00 | 4757 | Carrick Rangers vs Coleraine FC | 6.59 | 4.75 | 1.37 |
| 17:00 | 4893 | Eibar vs Leganes | 2.26 | 2.96 | 3.40 |
| 17:00 | 4998 | Warrenpoint vs Glenavon | 3.61 | 3.95 | 1.77 |
| 17:00 | 5412 | Oldham vs Barrow | 2.51 | 3.20 | 2.71 |
| 17:00 | 5557 | Bradford City vs Walsall | 1.69 | 3.53 | 4.90 |
| 17:00 | 5707 | Portadown FC vs Larne | 6.00 | 4.74 | 1.39 |
| 17:30 | 3592 | Almere City vs FC Oss | 1.64 | 4.01 | 4.40 |
| 19:00 | 1040 | Slovenia vs Malta | 1.19 | 6.59 | 14.98 |
| 19:00 | 1637 | Latvia vs Norway | 10.00 | 5.40 | 1.29 |
| 19:00 | 2737 | Ireland vs Azerbaijan | 1.56 | 3.90 | 6.19 |
| 19:00 | 3255 | Magdeburg vs Kaiserslautern | 1.77 | 3.59 | 4.23 |
| 19:00 | 3600 | Serbia vs Luxembourg | 1.25 | 5.82 | 11.03 |
| 19:00 | 4224 | Cyprus vs Russia | 8.01 | 4.51 | 1.40 |
| 19:15 | 2549 | FC Cartagena vs Real Sociedad B | 2.28 | 2.82 | 3.56 |
| 19:15 | 2739 | Tenerife vs Ponferradina | 1.99 | 2.96 | 4.24 |
| 19:45 | 1677 | Qatar vs Portugal | 7.03 | 5.23 | 1.38 |
| 21:45 | 1541 | Netherlands vs Montenegro | 1.17 | 7.38 | 14.95 |
| 21:45 | 1556 | Gibraltar vs Turkey | 80.11 | 17.02 | 1.01 |
| 21:45 | 2791 | Slovakia vs Croatia | 4.01 | 3.41 | 1.93 |
| 21:45 | 3243 | Ukraine vs France | 5.41 | 3.81 | 1.63 |
| 21:45 | 3540 | Bosnia and Herzegovina vs Kuwait | 1.44 | 4.50 | 7.00 |
| 21:45 | 4350 | Scotland vs Moldova | 1.17 | 6.80 | 17.01 |
| 21:45 | 4637 | Lanus vs Sarmiento Junin | 1.68 | 3.64 | 4.46 |
| 21:45 | 4957 | Faroe Islands vs Denmark | 25.91 | 9.17 | 1.10 |
| 21:45 | 5570 | Israel vs Austria | 3.45 | 3.20 | 2.19 |
| 22:00 | 1689 | Almeria vs Malaga | 1.72 | 3.36 | 5.13 |
| 22:00 | 1919 | Leones FC vs Union Magdalena SM | 2.07 | 3.07 | 3.50 |
| 22:00 | 2858 | Fuenlabrada vs Lugo | 1.95 | 2.96 | 4.44 |
| 23:00 | 1052 | Lala FC vs Metropolitanos | 2.95 | 3.39 | 2.17 |
| 23:00 | 5705 | Llaneros FC vs Club Cortulua | 2.34 | 2.88 | 3.12 |
| 23:10 | 3935 | Almirante Brown vs San Martin Tucuman | 2.22 | 2.90 | 3.34 |
| 23:15 | 5185 | Nautico PE vs Guarani SP | 2.37 | 2.95 | 3.00 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.




# MBAPPE AONDOLEWA KIKOSINI UFARANSA

**PARIS,** Ufaransa

MSHAMBULIAJI wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe ameachwa kwenye kambi ya timu ya Taifa ya Ufaransa baada ya kuumia kwenye mchezo wa Jumatano wa sare ya bao 1-1, dhidi ya Bosnia and Herzegovina.

'Les Bleus' tayari walikuwa bila nyota wa Chelsea, N'Golo Kante na mkali wa Bayern Munich, Corentin Tolisso, ambaye aliondolewa kwenye kikosi hicho, kwa sababu ya majeraha.

Taarifa ya timu ya Taifa ya Ufaransa ilieleza kuwa, mchezaji huyo hatakuwa tena kwenye kambi ya timu hiyo, baada ya kuumia nyama za paja.

Kikosi hicho cha kocha Didier Deschamps, kitacheza na Ukraine Jumamosi kabla ya kuivaa Finland Jumanne ijayo.

Licha ya kukosa huduma ya Mbappe, lakini ana wakali kama Thomas Lemar, Kingsley Coman, Moussa Diaby na Anthony Martial, huku safu ya ushambuliaji ikiongozwa na Karim Benzema na Antoine Griezmann.

Mbappe, sasa atarudi katika klabu yake ya PSG kuendelea na mazoezi mepesi kabla ya kurudi tena kwenye ligi.



# Chelsea yashtakiwa FA

**LONDON,** England

CHELSEA imeshtakiwa na Chama cha Soka cha England (FA), kwa kushindwa kuwadhibiti wachezaji wake wakati wa mchezo wa Jumamosi wa Ligi Kuu, dhidi ya Liverpool.

Shtaka hilo linahusiana na visa viwili baada ya uamuzi wa mwamuzi, Anthony Taylor kumtoa Reece James na kuipatia Liverpool penalti katika kipindi cha kwanza kutokana na beki huyo kuamuliwa kuwa alitumia mkono wake kwa makusudi kuzuia shuti.

Wachezaji wa Chelsea walijibu kwa hasira, huku mlinzi Antonio Rudiger na mlinda mlango Edouard Mendy wakionekana kufoka zaidi, na mzozo uliendelea hata baada ya mapumziko.

Blues hao wameshtakiwa kwa makosa mawili ya sheria ya FA E20.1 na imepewa hadi leo Ijumaa kujibu.

Chelsea iliongoza uwanjani Anfield kupitia bao la kichwa kutoka kwa Kai Havertz wakati Taylor alipotoa penalti, na Mohamed Salah alifanikiwa kuisawazishia Liverpool na mchezo kumalizika kwa sare ya 1-1.

Thomas Tuchel na Jurgen Klopp walikubaliana baada ya mchezo kwamba uamuzi wa jumla kutoa adhabu na kumtoa James ilikuwa adhabu kali.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# RONALDO APEWA JEZI NAMBA 7 YA CAVANI

**Nilikuwa sina uhakika kama nitapata tena jezi namba saba, hivyo napenda kutoa shukrani kwa Edi (Cavani)...**

**MANCHESTER,** England

CRISTIANO Ronaldo atavaa jezi namba saba kwa Manchester United, klabu hiyo imethibitisha.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36, ameichukua namba hiyo, ambayo alivaa wakati wa kipindi chake cha kwanza kucheza hapo Old Trafford, kutoka kwa straika wa Uruguay, Edinson Cavani - ambaye sasa atavaa namba 21.

Ronaldo ataanza mazoezi na 'Mashateni Wekundu' hao mara tu atakapomaliza siku tano za kujitenga kutokana na sababu ya sheria za mlipuko wa virusi vya corona nchini Uingereza.

Alhamisi aliachiwa na timu ya taifa, ili aweze kwenda Uingereza kuanza kujitenga kwa siku tano.

"Nilikuwa sina uhakika kama nitapata tena jezi namba saba, hivyo napenda kutoa shukrani kwa Edi (Cavani), kwa uamuzi wake wa kukubali kuiachia," alisema Ronaldo.

"Nyota wa Ureno atavaa jezi namba saba, ambayo aliivaa katika kipindi chake cha kwanza hapa United na sasa tunaweza kuthibitisha kwamba, Ronaldo atavaa tena jezi hiyo," ilisema taarifa ya United kupitia kwenye tovuti yake.

Ronaldo alikamilisha uhamisho wa kushitukiza kwenda Old Trafford katika siku ya mwisho ya kufungwa kwa dirisha la uhamisho na anatarajia kuwachezea kwa mara ya kwanza 'Mashetani' hao katika mchezo wa Ligi Kuu England dhidi ya Newcastle, Septemba 11.

Ronaldo aliweka rekodi ya kuwa mfungaji bora wa wakati wote kwenye timu ya taifa, wakati alipofunga mara mbili dhidi ya Jamhuri ya Ireland, Jumanne, lakini alionyeshwa kadi ya njano kwa kuvua jezi.

Ronaldo sasa amefikisha mabao 111 kwa timu ya Taifa ya Ureno na kuipiku rekodi ya Ali Daei, ambaye alifunga mabao 109 kwa timu ya Taifa ya Iran kati ya mwaka 1993 na 2006.

## ZISIKUPITE

### AURIER HUYOOO ARSENAL
MLINZI wa Ivory Coast, Serge Aurier mwenye umri wa miaka 28, atakuwa huru kuhamia Arsenal baada ya kumaliza mkataba wake kule Tottenham Hotspur siku ya mwisho ya uhamisho. ***(Sky Sports)***

### KOUNDE AIKASIRIKIA SEVILLA
BEKI wa Ufaransa, Jules Kounde mwenye umri wa miaka 22, ana hasira na Sevilla kwa kutomuuza kwenda Chelsea. ***(Spanish Football Podcast, via Express)***

### MADRID YAKOMAA KWA HAALAND
REAL Madrid iko tayari kumsaka mshambuliaji wa Norway na Borussia Dortmund, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 21 na mshambuliaji wa Ufaransa na Paris St-Germain mwenye umri wa miaka 22, Kylian Mbappe msimu ujao. ***(Marca, via Mail)***

### POGBA ATAKIWA MADRID
REAL Madrid pia inavutiwa kumleta kiungo wa kati wa Ufaransa, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 28, ili atue pale Bernabeu kutoka Manchester United. ***(Marca, via Manchester Evening News)***

### CHELSEA YAKWAMA TENA
MPANGO wa Chelsea wa kumuwania Erling Haaland umepata pingamizi baada ya kuambiwa watalazimika kulipa pauni 825,000, kwa wiki kwa mshahara wake. ***(Mirror)***

### SOLSKJAER ALIZUIA NYOTA
KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, alizuia wachezaji watano kuondoka Old Trafford siku ya mwisho ya kufungwa kwa dirisha la uhamisho wa majira ya joto. ***(Mirror)***

### WALKER-PETERS AWANIWA
KLABU ya Everton ilimfuatilia mlinzi wa England na Southampton mwenye umri wa miaka 24, Kyle Walker-Peters katika siku za mwisho za usajili. ***(Telegraph, via Football Transfer Tavern)***

### JUVE YAFUNGUKA KWA CAVANI
JUVENTUS ilikataa nafasi ya kumsajili mshambuliaji wa Uruguay, Edinson Cavani mwenye umri wa miaka 34, kutoka Manchester United muda mfupi baada ya mshambuliaji wa Ureno Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 36 kuondoka klabuni hapo. ***(Mirror)***

### WOLVES KURUDI KWA TRAORE
KLABU ya Wolves inapanga kufuatilia tena hali ya mkataba wa winga, Adama Traore baada ya kukataa mkataba mara mbili kutoka Tottenham Hotspur kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania. ***(Birmingham.Live)***

### WAKALA WA DIAZ ASHANGAA
WAKALA wa Mariano Diaz amesema kuna "kitu cha kushangaza kilichotokea" kumzuia mshambuliaji huyo wa Hispania mwenye umri wa miaka 28, kujiunga na Valencia kutoka Real Madrid. ***(El Partidazo de Cope, via Football Espana)***

# HABARI MICHEZO

## Nakupenda Marathon Zanzibar Oktoba 16

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Ali Khamis Juma, amesema, kuwapo kwa mashindano ya 'Nakupenda Marathon' kutaisadia kutangaza utalii wa Zanzibar kwa wageni watakaoshiriki.

Akizungumza katika uzinduzi wa Kampeni ya Nakupenda Marathon, iliyofanyika katika Ukumbi wa Zura Maisara Mjini Unguja, alisema mashindano hayo yanaweza kusaidia watoto wa kike kupata taulo za kike, kwani waandaaji wamelenga kwa kiasi kikubwa katika kumsaidia mwanamke.

Aidha, alisema wizara imefarajika kuona hatua hiyo ambayo imemwezesha mtoto wa kike kuendelea kupata masomo kuweza kwa kiasi kukubwa kuhudhuria masomo wakati akiwa katika hedhi.

Sambamba na hilo, aliwaomba wafadhili wengine kuwa na mwamko wa kusaidia mtoto wa kike, ili kuona anapata huduma hiyo ya taulo.

Kwa upande wa ZURA Nakupenda Marathon 2021, Benedict Anthony, alisema mashindano hayo, yanatarajiwa kufanyika Oktoba 16, mwaka huu katika Uwanja wa Mnazimmoja na kuwataka wananchi kushiriki mbio hizo, ambapo kabla ya kilele kutakuwapo ufanyaji wa usafi katika maeneo mbalimbali ya miji.

## Mtuli amrithi Sape Kocha Polisi Z'bar

**Na Hawa Abdallah, Zanzibar**

UONGOZI wa timu ya Polisi Zanzibar inayoshiriki Ligi Kuu Zanzibar, imemtangaza Ali Mtuli, kuwa Kocha Mkuu wa timu hiyo kuelekea msimu mpya wa 2021/22.

Kocha Mtuli alikuwa Mkurugenzi wa Ufundi wa timu ya Polisi Tanzania na pia aliwahi kuinoa Polisi ya Zanzibar kwa misimu ya nyuma.

Akizungumza na gazeti hili Katibu Mkuu wa timu ya Polisi Zanzibar, Haji Issa Kidali, alisema wameamua kumrejesha Mtuli kukinoa kikosi hicho, ili kiwe na mafanikio ikilinganishwa na msimu uliopita, ambao haikufanya vizuri hadi kufikia hatua ya kuponea chupuchupu kushuka daraja.

Alisema kocha huyo ambaye tayari yupo Zanzibar akitokea Polisi Tanzania ya Tanzania Bara, mapema wiki ijayo atatangaza wasaidizi wa benchi lake la ufundi.

Akizungumzia kuhusu kocha aliyekinoa kikosi hicho msimu uliopita, Yusup Sape, Kidali alisema hatma yake ipo mikononi mwa Mtuli kupitia benchi lake la ufundi atakalolitangaza.

# POULSEN ATOA SABABU STARS KUISHIKA DR CONGO

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa timu ya Taifa ya Tanzania, 'Taifa Stars', Kim Poulsen, amesema awali wachezaji wa timu ya Taifa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo waliwadharau na kwa kiasi kikubwa ilisababisha wawe kwenye wakati mgumu, hadi walipobadilika baadaye.

Akizungumza juzi, baada ya kumalizika kwa mechi ya kusaka tiketi ya kucheza fainali za Kombe la Dunia nchini Qatar mwakani, kocha huyo raia wa Denmark alisema ameridhishwa na sare iliyopatikana, kwa sababu walicheza na timu ngumu yenye wachezaji wakubwa.

"Ilikuwa mechi ngumu kucheza ugenini na timu ya DR Congo, timu kubwa kwenye viwango vya soka. Ilikuwa na wachezaji wakubwa waliocheza soka la kulipwa Ulaya na sehemu zingine nje ya nchi yao, mwanzo walionekana kucheza kwa kutudharau wakidhani Tanzania haiwezi kucheza kama ilivyocheza. Sisi tuliwaheshimu, lakini wao walicheza kwa dharau, nadhani baadaye walipoona mambo yanazidi kuwa magumu walibadilika," alisema kocha huyo.

Naye golikipa namba moja wa Stars, Aishi Manula alisema mechi ilikuwa ngumu kutokana na mazingira ya kucheza ugenini.

"Tulikuwa tunacheza na wachezaji wakubwa, lakini ukitaka na wewe kuwa mkubwa, lazima ucheze mechi kubwa na wachezaji wakubwa, tunashukuru kupata pointi moja ugenini," alisema.

Kwenye mechi hiyo ya Kundi J, iliyochezwa mjini Lubumbashi kwenye uwanja unaomilikiwa na klabu ya TP Mazembe, wenyeji walianza kupata bao dakika ya 23 likifungwa na Dieudinne Mbokani, Simon Msuva akiisawazishia Stars dakika ya 35.

Stars itacheza mechi nyingine nyumbani dhidi ya Madagascar Jumanne ijayo, ambayo ilichapwa bao 1-0 nyumbani dhidi ya Benin.

**KIMBIZA...**



Mshambuliaji wa Simba Queens, Flavine Mawete (kulia), akiwatoka mabeki wa FAD ya Djibouti katika mechi ya Kundi A ya Ligi ya Mabingwa Afrika Ukanda wa CECAFA iliyochezwa kwenye Uwanja wa Moi Kasarani jijini Nairobi, Kenya jana. **PICHA : SOMOE NG'ITU**

## *Biashara kutafutia kasi ya CAF Daraja la Pili*

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Biashara United, ambayo inajiandaa na mchezo wake wa Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya FC Dikhil ya Djibouti utakaopigwa Septemba 10, mwaka huu nchini humo, itajipima ubavu kuelekea mechi hiyo dhidi ya Cotco FC inayoshiriki Ligi Daraja la Pili mkoani Mwanza, imeelezwa.

Biashara United, ambayo iliweka kambi jijini Mwanza kujiandaa na michuano hiyo ya kimataifa, itautumia mchezo utakaopigwa Uwanja wa Kumbukumbu ya Karume, Musoma leo, kutambulisha kikosi chake cha msimu ujao wa 2021/22.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa klabu hiyo, Frank Wabare, alisema anashukuru wamefanikiwa kumaliza salama kambi yao, ambayo walikaa kwa muda wa siku 16 kwa lengo la kujiandaa na mchezo huo wa kimataifa pamoja na msimu ujao wa Ligi Kuu Bara.

"Leo asubuhi tumeanza safari ya kurudi Mara, kwa ajili ya kujiandaa na mchezo wetu wa kirafiki, ambao tutaucheza kesho (leo) na timu ya Cotco FC ya Mwanza na kutambulisha wachezaji wetu kwa wananchi," alisema Wabare.

Meneja huyo alisema baada ya kumaliza mchezo huo, wataanza kujipanga, kwa ajili ya safari ya kuelekea Dar es Salaam keshokutwa ambapo Septemba 6, wachezaji wote pamoja na viongozi watafanyiwa vipimo vya maambukizo ya virusi vya corona kabla ya kuelekea nchini Djibouti Septemba 7, mwaka huu.

Aliongeza kuwa mchezo huo wa kirafiki wanauchukulia kama maandalizi kuelekea katika mechi yao ya ugenini, ambayo anatumaini itakuwa ngumu na yenye ushindani mkubwa, hivyo anaomba Watanzania wazidi kuwaombea wafanye vizuri.

Alisema kambi ya muda mrefu waliyoweka Mwanza imewasaidia kwa kiasi kikubwa wachezaji na kwamba kwa sasa akili zao na nguvu zote wanaziwekeza katika michezo ya kimataifa pamoja na mashindano ya msimu ujao wa Ligi Kuu.

# Michezo

Jumamosi Septemba 4, 2021
Nipashe



Ronaldo apewa jezi namba 7 Utd

KIWANGO...



Wachezaji wa Simba wakitambulisha moja ya jezi mpya za msimu wa 2021/22, ambapo mashabiki wa timu hiyo wanasema "Timu Kiwango, Jezi Kiwango". **PICHA: SIMBA**

# SIMBA DAY NI 'ONE TEAM, ONE DREAM'

## Jezi mpya 'hakunaga' kama hizo, zakimbiza kila kona, Simba Queens nayo yapiga mtu 10, hat-trick tatu...

**Saada Akida, DAR na Somoe Ng'itu, NAIROBI**

NI "Kiwango"! Kauli hiyo ndiyo iliyotawala mdomoni mwa mashabiki na wadau wa soka nchini wakati wakizungumzia na kununua kwa wingi jezi za msimu mpya wa 2021/22 za Klabu ya Simba baada ya kuanza kuuzwa rasmi jana kote nchini kuelekea uzinduzi wake utakaofanyika leo jijini Dar es Salaam.

Aidha, klabu hiyo imesema kuelekea Simba Day Septemba 19, mwaka huu, wamekuja na Slogan mpya ya 'One Team, One Dream'.

Jana jezi hizo zilianza kuuzwa rasmi kote nchini na kushambuliwa kwa wingi na mashabiki wa timu hiyo huku wengi wakionyesha kuvutiwa zaidi na 'uzi' wa rangi nyeupe, lakini zile aina ya 'Form Six', maalum kwa mtoko, ndizo zilizoshambuliwa na kumalizika katika maduka mbalimbali jijini Dar es Salaam kabla ya wasambazaji kuongeza zingine.

"Kweli hizi jezi ni zaidi ya kiwango, 'hakunaga' kama hizi, huwezi kuzifananisha na zile za..., ambazo ni za kiwango cha chini, mwaka huu Simba imetisha kwa kuleta uzi kiwango," walisikika mashabiki wa timu hiyo wakati wakinunua jezi Sinza, Dar es Salaam.

Wakati huo huo Kaimu Mkuu wa Kitengo Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ezekiel Kamwaga, ameweka wazi kuwa kesho watatangaza sehemu kikosi chao kitakapoweka kambi ya awamu ya pili kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara na Ligi ya Mabingwa Afrika msimu wa 2021/22.

Simba haijaweka wazi kambi hiyo itakuwa wapi, lakini taarifa za ndani zilizolifikia gazeti hili zinasema kuwa kikosi kinatarajiwa kwenda Karatu, Arusha kujiandaa na msimu mpya na kurejea Dar es Salaam siku chache kabla ya kilele cha tamasha la Simba Day litakalofanyika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Septemba 19, mwaka huu.

Kamwaga alisema baada ya timu kurudi kutoka Morocco wachezaji walipewa mapumziko ya siku chache na leo wanarejea na kuondoka moja kwa moja kuelekea sehemu ambayo kumepangwa kambi hiyo.

"Ni wapi? Tutaweka wazi kesho (leo) kila kitu kinaenda vizuri ikiwamo kambi ya awali ya pili na tunatarajia kikosi kurejea siku chache kabla ya kilele cha tamasha letu la Simba Day," alisema Kamwaga.

Aidha, alisema maandalizi ya tamasha hilo yanaenda vizuri, na kuanzia Septemba13, mwaka huu, itakuwa ni Wiki ya Simba kwa mashabiki na wanachama wa klabu hiyo kuanza kufanya shughuli huku kuanzia jana tiketi za kushuhudia Simba Day zikianza kuuzwa.

"Lengo kubwa la kuuza tiketi mapema ni kuepuka usumbufu na msongamano wa ununuzi wa tiketi, bei ya tiketi hizo ni Sh. 5,000 kwa mzunguko, VIP B na C ni Sh. 20,000, VIP A Sh. 30,000 na Platinum Sh. 200,000 ambapo zitajumuisha sehemu maalum ya kukaa, zawadi ya jezi mpya, chakula cha mchana na usafiri wa kumfikisha uwanjani na kumrudisha katika makutano.

"Msimu huu tumekuja na Slogan mpya ya Simba Day 2021, ambayo ni 'One Team, One Dream'. Twendeni wenye nchi, mwaka huu tunaenda na kauli hiyo, mashabiki na wadau wa Simba wanatakiwa kununua tiketi kwa sababu siku hiyo si ya kukosa," alisema Kamwaga.

Kuhusu timu itakayocheza mechi ya kirafiki siku hiyo, Kamwaga alisema: "Tumepokea maombi mengi kutoka timu mbalimbali kutaka kuja Simba Day, lakini cha kuwathibitishia Wanasimba, timu itakayokuja lazima iwe imechukuwa taji la Ligi ya Mabingwa Afrika mara tatu".

Katika hatua nyingine timu ya Wanawake ya Simba, Simba Queens imetinga hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Ukanda wa CECAFA baada ya kupata ushindi wa mabao 10-0 dhidi ya FAD kutoka Djibouti katika mechi ya Kundi A iliyochezwa Uwanja wa Moi Kasarani jijini Nairobi jana mchana.

Kwa ushindi huo, Simba Queens imeongoza Kundi A kutokana na tofauti kubwa ya mabao baada ya kufikisha pointi saba sawa na Lady Doves FC ya Uganda ambayo jana ilipata ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Mabingwa wa Ligi ya Wanawake Burundi, PVP FC.

Mabao ya Simba Queens katika mchezo huo wa jana yalifungwa na Flavine Mawete, Oppa Clement na Aisha Juma ambao walifunga hat-trick kila mmoja na Aisha Djafar akipachika moja na kukamilisha karamu hiyo ya magoli.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >